Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

لا اله الا الله محمد رسول الله

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika Wake humsalia Mtume; enyi mlioamini, msalieni (Mtume) na mwombeeni amani. Kwa yakini wale wanaomwudhi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, Mwenyezi Mungu Amewalaani katika dunia na Akhera, na Amewaandalia adhabu ifedheheshayo. (33:57-58)

JUZU 74 No. 183 | DH.QA'DA/DH. HJ 1436 AH | SEPTEMBA 2015 | IKHA 1394 HS | BEI TSH. 500/=

Jumuiya yazidi kubarikiwa na Allah - Khalifa Mtukufu

Na Mwandishi Wetu

Akitoa hotuba ya Ijumaa mara baada ta jalsa Salana ya Uingereza mwaka 2015, Khalifa Mtukufu alielezea Juu ya Baraka ambazo Allah ameendelea kuibariki Jamaat Ahmadiyya ndani ya kipindi cha mwaka uliopita. Katika hotuba hiyo Huzur Aqdas alisema:

Barua za pongezi na nukushi (fax) zinaendelea kupokelewa kutoka sehemu mbalimbali za dunia kuhusu mafanikio ya Jalsa Salana mwaka huu zikieleza faida zilizopatikana kwa kuangalia Jalsa kupitia MTA. Mafanikio hasa ya Jalsa yanapatikana iwapo kila kinachoonekana na kusikika kitakuwa ni chanzo cha mtu kujipamba kiroho.

Kwa hakika hakuna mjadala wa masuala ya kisiasa au ya kidunia katika Jalsa, wakati baadhi ya wageni wasio Waahmadiyya na wasio Waislamu walipozungumza kwa kifupi wengi wao wamevutiwa na mazingira ya kiroho yanayoonekana kwenye Jalsa na wametoa maoni yao kusifia mafundisho ya Jamaat. Jalsa bila shaka ina mafanikio makubwa iwapo kila kinachozungumzwa kitatekelezwa na wanajamaat. Vinginevyo sifa zote zitolewazo na wageni zitakuwa ni sifa za juu juu tu. Kuna haja ya kuwepo mfanano kati ya hali ya nje na ya ndani ya muumini.

Dunia imeanza kutusikiliza. Waahmadiyya na wasio

Endelea uk. 2

Sakata la Wakimbizi kutoka Mataifa ya Kiarabu: Ladhihirisha hali ya Umma wa Kiislam ilivyo mbaya

Na Abdulrahman M. Ame
Dar es Salaam

Hivi karibuni dunia imeshuhudia wimbi kubwa la wakimbizi wakitokea baadhi ya mataifa ya Bara Arabu kuelekea mataifa ya bara la Ulaya.

Sababu kubwa ya wimbi hilo la wakimbizi inayoelezwa ni vita kali iliyoshamiri katika mataifa ya Syria na Yemen ambako kuna mtafaruku mkubwa wa kugombania madaraka.

Wakati ambapo Saudia Arabia imeamua kuingia vitani kumsaidia rafiki yake rais Ali Abdallah wa Yemen na hivyo kusababisha maangamizi makubwa kwa raia, kwa upande wa Syria hali ni mbaya zaidi kwani vita yenye sura ya wenyewe kwa wenyewe imeshamiri katika kila kona ya nchi hiyo. Kuna makundi yanayotafuta kumuangusha rais Bashar Al Asad lakini pia kuna makundi yanayopigana kumsaidia na mengine yanayomshambulia yeyote asiyekubaliana na idikadi zao. Ukitilia maanani ugomvi baina ya makundi ya kishia na yale ya kisuni hasa sakata la ISIS hali ya Syria inachukua sura ya kutisha kabisa. Kwa ujumla hali ya Syria ni mbaya sana na ya kutishia sio uhai wa taifa la Syria tu bali usalama wa dunia nzima, kwani ukiongeza tatizo la mataifa yenye nguvu la kuunga mkono upande wa serikali ya Syria au wapinzani wake, hali inaweza kuwa mbaya zaidi hadi kupelekea vita ya tatu ya Dunia.

Taifa la Syria ni nchi iliyo na historia kubwa na ndefu kabla na baada ya kuja Islam. Katika zama za hadhi ya Uislamu (Golden age of Islam) Syria ilishawahi kuwa Makao makuu ya Dola la Kiislam.

Katika hadithi za Mtukufu Mtume s.a.w. kuna kutajwa kwingi kwa njia ya ajabu kuhusu taifa la Syria kwamba litakuwa kitovu cha ishara za Kiungu katika zama za mwisho.

Kwa mfano inaripotiwa kwamba mara kadhaa Mtume s.a.w. alipokuwa akimaliza sala alikuwa akiketi kuelekea upande wa mji mkuu wa Syria Damascus na alikuwa akisema yeye kwa kuelekea huko anaipata harufu ya Masihi na Mahdi ambaye atashuka upande wa mwelekeo wa Mashariki ya mji mkuu wa Syria - Damascus.

Aidha Mtukufu Mtume s.a.w. alishawahi kusema mara kadhaa kwamba, ishara moja ya kiama ni moto mkubwa utakaoambatana na fitina za Dajjal na Yaajuja na Maajuja utakaotokea katika ardhi ya Syria.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. naye aliwahi kupata ufunuo kuihusu Syria uliosema "Maangamizi yameiangukia Damascus"

Mwenyezi Mungu Ndiye Ajuaye zaidi maana halisi ya kutimia kwa bishara hizi, hata hivyo tunaweza kusema kwamba ukweli wa bishara hizi unaweza kujitokeza kwa namna mbalimbali na mara kadhaa. Kwa mfano mnamo mwaka 1925 serikali ya Ufaransa ikijirabu kuzuia vuguvugu la kudai uhuru lililokuwa likiongozwa na Jumuiya ya Kidruze huko Syria, iliushambulia mji wa Damascus kwa masaa 57 ambapo karibu mji mzima ulibaki kuwa vumbi na magofu na watu wanaokisiwa kuzidi 8000 kupoteza maisha.

Lakini leo hali ya Syria ni ya kutisha zaidi. Malaki ya watu tayari wamepoteza maisha, malaki kujeruhiwa na mamilioni kuwa wakimbizi ama ndani au nje ya nchi yao.

Bila shaka kila Muislam anahuzunishwa sana na hali hiyo lakini sisi Waahmadiyya tunahuzunika zaidi kwani hali hiyo mbaya iliyoyazunguka mataifa ya Kiislamu inaifanya

Endelea uk. 2

Mapenzi ya Mungu
Maoni ya Mhariri

Hali ilivyo mbaya

Kutoka uk. 1

kazi yetu ya kuutangaza ujumbe wa Islam na uzuri wake duniani kuwa ngumu zaidi na inayohitaji kutolewa maelezo zaidi.

Dunia, hasa ya wasio Waislam, inapigwa na butwaa kwa kuona hali ilivyo kwenye mataifa haya, kwani wanashindwa kuoanisha kati ya kile kinachotokea na kile tunachowaeleza kuwa ndio mafundisho sahihi ya Islam.

Kwa kuona hali hii, Khalifa Mtukufu a.t.b.a. ameendelea kutuagiza mara kadhaa kwamba tuongeze maombi yetu kwa ajili ya Umma wa Kiislam na wanadamu kwa ujumla, ili mgogoro huu usiendelee kuipaka matope Islam bali pia usije ukafikia kuwa chanzo cha vita kuu ya tatu ya dunia.

Hata hivyo pamoja na masikitiko yetu na maombi yetu, sakata hili linatupa darsa kubwa la kujifunza juu ya hali ya Waislamu ilivyo mbaya leo duniani hali ambayo inawasuta wale Waislamu ambao kwa karne nzima sasa wamekuwa wakihoji haja ya Mwenyezi Mungu Kumtuma Mjumbe wa kuja kuturejesha kwenye usahihi wa Islam.

Waislamu wanaoipinga Jumuiya hii ya Masihi Aliyeahidiwa wameendelea kuhoji haja ya kuja kwa mtu wa aina yoyote kutoka kwa Mungu kuufundisha Uislamu kwa madai kwamba wao ni warithi wa Mtume na hivyo wanaweza kutatua matatizo yao wenyewe na kurekebisha hali zao bila ya msaada wa ufunuo wowote wa kimbingu. Lakini anaweza kuhoji mwenye kuhoji:

- Uko wapi udugu wa Kiislam unaooneshwa na mataifa ya Kiarabu mbele ya mafundisho ya Islam ya udugu, upendo na kuhurumiana miongoni mwa Waislamu?

Wakati Waislamu wa Syria na Yemen wanaojaaliwa kuvuka bahari ngumu ya Atlantik wanapokelewa kwenye baadhi ya mataifa ya Ulaya kama wakimbizi, mataifa ya Kiislam yaliyo jirani na Syria na Yemen yakikataa kata kata kupokea hata mkimbizi mmoja, mbele ya fundisho hili: **Waislamu ni wenye kuhurumiana wao kwa wao** (48:30).

- Yako wapi mataifa ya Kiislam yausuluhishe mgogoro wa Syria sawa na fundisho la Kiislam:

Na ikiwa makundi mawili katika waaminio wanapigana, basi fanyeni suluhu kati yao; na ikiwa moja la hayo limemrukia mwenziwe, basi lipigeni lile lililorukia mpaka lirudie kwenye amri ya Mwenyezi Mungu. Na kama likirudi, basi yapatanisheni baina yao kwa uadilifu, na hukumuni kwa haki. Hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wanaohukumu kwa haki. Hakika Waaminio ni ndugu, basi fanyeni suluhu baina ya ndugu zenu (49:10-11).

- Liko wapi fungamano la mataifa ya Kiislam, OIC, ambalo moja ya malengo ya kuundwa kwake ni kukuza udugu na umoja wa Kiislam huku fungamano hilo likidai kwamba eti 'Makadiani' (Ahmadiyya) ndio wanaosababisha mtengano wa Waislamu.

- Wakati Islam ni dini inayosisitiza uadilifu kwa kiwango cha hali ya juu: ... **Na uadui wa watu usiwashawishini ya kwamba msifanye uadilifu. Shikeni adili, hiyo ni karibu sana na utawa** ... (5:9). Uko wapi leo uadilifu kwenye mataifa ya Kiarabu katika kulishughulikia swala la mgogoro wa Syria na Yemen?

- Hebu ona leo mataifa makubwa ya Kiislam yanavyosaidiana katika uovu wa kuwaangamiza waislamu wenzao mbele ya fundisho lenye nguvu la Qurani tukufu ... **Na saidianeni katika wema na utawa, wala msisaidiane katika dhambi na uasi**.... (5:3).

- Waislamu wametajwa kuwa ni umati bora kuliko wengine wote: **Ninyi ni umati bora mliotolewa kwa ajili ya watu** - (3:111), lakini leo upo wapo ubora wa Waislamu, iko wapi heshima yao, iko wapi ghera ya viongozi wa mataifa ya Kiislamu, kilichobaki kwao ni kuyasujudia mataifa yenye nguvu na kuyaomba msaada wa kutatuliwa matatizo yao. Wenyewe hawajiwezi, hawajitambui!

Bila shaka hali ni ya kusikitisha mno. Lakini hali ni ya kusikitisha zaidi pale ambapo pamoja na hali hiyo, bado Mislamu anasimama kifua mbele akidai kwamba hana haja ya nabii. Nabii wa Mwenyezi Mungu wa kuwaonyesha Waislamu njia ya kupita katika giza hili totoro, njia ya kutatua mitafuruku yao, njia ya kuleta umoja wao na njia ya kurudisha heshima yao na nguvu yao.

Hali ya Syria, pamoja na bishara nyingi iliyoizunguka inaitangazia dunia na hasa dunia ya Kiislam kwamba hali yao ni mbaya sana, hawawezi kujisaidia kwa chochote na bila ya msaada kutoka mbinguni uletwao kwa njia ya unabii hawana njia yoyote ya kuokoka. Mgogoro wa Syria na mataifa mengine ya Kiislam ni dalili iliyo wazi kwamba Mwenyezi Mungu ameshatimiza ahadi Yake Aliyompa Mtume wake mpendwa Muhammad s.a.w. ya kumtuma Masihi na Mahdi ili kuuokoa umati wake.

Mwenyezi Mungu Amsaidie kila Muislamu na kila mwanadamu kuuelewa ukweli huu.

Mwenyezi Mungu Aiepushe dunia dhidi ya maangamizi na Ajaalie amani na upendo vitawale badala ya chuki na vita.

Jumuiya yazidi kubarikiwa na Allah

Kutoka uk. 1

Waahmadiyya duniani kote wanaangalia Jalsa Salana kupitia MTA, hasa ile ya UK inaangaliwa kwa makini zaidi. Mamia kwa maelfu ya fedha yanatumika kwenye MTA, ili kwamba kila mwanajumuiya awe na nafasi ya kuelewa malengo yetu. Furaha yetu isiwe kuhudhuria Jalsa tu au kuangalia MTA. Wale wanaoshiriki Jalsa wao wenyewe na wale wanaoangalia kupitia MTA wajitahidi kuyaingiza kwenye matendo yale wanayoyasikia kwenye Jalsa na pia tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia njia za kupata mafanikio ya kiroho kwenye kipindi hiki cha watu kuielekea dunia.

Njia za mawasiliano za kidunia zinatuwezesha kupata maendeleo ya kiroho iwapo tutazitumia ipasavyo. Hili lilitabiriwa miaka 1400 iliyopita kwamba maendeleo ya kielimu ya dunia yatasaidia imani. Hili linatakiwa lituelekeza zaidi kwa Mwenyezi Mungu na kumshukuru. Mwenyezi Mungu anasema: ... Kama mkishukuru, bila shaka Nitawazidishieni ... (14:8). Somo la shukurani linatuonesha kwamba tumshukuru Mwenyezi Mungu na tuwashukuru watu pia. Kama vile Mtume Mtukufu s.a.w. alivyosema: Asiyeashukuru watu hamshukuru Mwenyezi Mungu pia.

Watoa huduma kwenye Jalsa waliweza kujipanga na kutoa huduma katika idara kadhaa ikiwemo MTA. Wahudumu hawa walikuwa ni kinababa, kinamama, watoto, wazee na vijana pia, ambao walijitahidi kwa kadri ya uwezo wao. Wahudumu hawa wanatoka kwenye nyanja mbalimbali za maisha, wakiwemo Maafisa, madaktari, wahandisi na fani zingine, lakini wote wamefanya kazi zao bila kujali hata kwa mbali fani zao. Baadhi yao kwa furaha walisimama kwenye moto wakipika masifuria makubwa, hata vijana wa umri mdogo nao pia wameifanya kazi hii kwa furaha. Makundi ya kinababa na kinamama yamesafisha vyoo bila mnato, wengine wakiwaendesha wazee na walemavu kwenye vigari kutoka mahala pamoja hadi pengine. Watoto nao walikuwa wakihudumia kugawa maji ya kunywa wakati wa joto huku makundi ya kinababa na kinamama wakiwahudumia watu kupata chakula.

Pia kuna idara muhimu na yenye mambo mengi ya ulinzi. Kifupi kila mtoa huduma ama akiwa mzoefu au mpya kwenye huduma fulani, alijitahidi kwa subira kubwa na kwa uwezo wake wote kutoa huduma aliyopangiwa. Pia kuna jukumu la kuanua jamvi baada ya Jalsa. Kulinyesha mvua kubwa baada ya Jalsa ambayo imeongeza ugumu wa kazi, lakini Khuddam wameifanya kazi hiyo kwa bidii kubwa kama walivyofanya wakati wa ujenzi. Kazi ya kukunja mazingira ya Jalsa ni ya changamoto kubwa kwani kuna kipindi maalum kinachotolewa na Manispaa. Kushindwa kukunja ndani ya kipindi tulichoagizwa kunaweza kupelekea kunyimwa ruhusa baadae.

Mwaka huu Khuddam kutoka Canada wameungana na Khuddam wa UK kwenye ukunjaji na hilo limesaidia sana kazi. Wote hao wanastahili shukurani zetu. Kwa hakika tunawashukuru wahudumu wote. Pia kwa ajili ya wanajumuiya, Huzur Aqdas aliwashukuru wageni wote wa Jalsa kwa ushirikiano wao na kwamba mwaka huu kumekuwa na malalamiko machache sana.

Waheshimiwa wengi waliokuja kwenye Jalsa wamesifia na kushukuru. Mwenyezi Mungu ameyafunika mapungufu yetu na wageni wameyaona yale yaliyo mazuri.

Waziri kutoka Uganda alisema kuwa alishangazwa na utaratibu wa Jalsa jinsi ilivyopangika, na ameona kana kwamba wale wanaohudumia ni kama malaika. Hata kama kuna haja iliombwa wakati ambao ni mgumu, wao waliitimiza kwa furaha. Alisifia maonyesho mbalimbali katika Jalsa na alisema kuwa kwa namna Jumuiya inavyofanya kazi itaweza kuishinda dunia katika miaka michache ijayo. Alisifia ujumbe wa amani uliotolewa kwenye Jalsa.

Hakimu kutoka Ufaransa ya Guyana alisema kuwa alipokuwa anakuja kwenye Jalsa alikuwa na maumivu katika mguu wake ambapo kimiujiza yakapotea kwa haraka mara tu alipofika kwenye Jalsa.

Mwenyekiti wa kituo kimoja cha TV huko Nigeria ambaye ameshawahi kwenda Hijja alisema kuwa alijisikia alikuwa katika bonde la Arafat. Alisema hajawahi kuona jambo kama hilo kabla na pia hajawahi kuona kiwango kisicho na mfano cha utii kama ambacho wanajumuiya wanakionesha kwa Hazrat Khalifatul Masih.

Hakimu kutoka Congo alisema kuwa akiwa hakimu alikuwa na ufahamu wa kupambanua uhalisia kutoka kwenye usanii. Alisema ameiona Jalsa kuwa dhihirisho la lile alilokuwa amesikia kabla kuhusu Jumuiya na kukuta ni picha halisi ya Uislamu.

Makamu wa Rais wa Sierra Leone alisema kwamba Jalsa ilikuwa tukio kubwa. Meya kutoka Sierra Leone alisema siku tatu za Jalsa walikuwa wamejichimbia katika kambi ya kiroho na kusababisha kuleta mabadiliko ya kimapinduzi ndani yake.

Naibu Waziri wa Michezo wa Sierra Leone alisema Jalsa ilikuwa ni uzoefu wa ajabu. Alisema hajawahi kuona wageni kuheshimiwa kama wanavyoheshimiwa katika Jalsa.

Spika wa Bunge la Benin alisema aliona upendo mkubwa Waahmadiya walionao kwa Khalifa wao. Alisema popote alipotazama alikuta mipango iliyopangwa vizuri sana na licha ya idadi kubwa ya mahudhurio mipango ya Jalsa ilikuwa bora kabisa. Hili lilikuwa ni tukio la kipekee.

Ahmadia mmoja kutoka Argentina alisema kuwa yeye alikuwa anatafuta imani ya kweli kwa miaka kumi iliyopita na sasa anashukuru ameipata. Alivutiwa sana na mipango ya Jalsa hasa ushiriki wa vijana. Pia alishiriki kwenye tukio la International Bai'at na kusema huo ulikuwa ni wakati wa furaha kubwa katika maisha yake. Alifurahi pia kuwa Ahmadia wa kwanza kutoka Argentina.

Mgeni mmoja kutoka Japan alisema kuwa ukarimu na huduma ya kujitolea ya Jalsa itakuwa kumbukumbu isiyosahaulika kwake. Alisema Jalsa ilikuwa mfano halisi wa UNO (Umoja wa Mataifa) kwa watu kutoka duniani kote kukutana pamoja. Mgeni mwingine kutoka Japan alisema amekuwa akiangalia imani tofauti kwa miaka kumi

Endelea uk. 4

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Mafundisho yaliyo Bora kabisa

Kutoka Maandishi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Hadhrat Ahmad, Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema:

.... Basi enyi watu wote mnaojihesabu katika jamaa yangu! Hamtahesabiwa mbinguni katika jamaa yangu mpaka mtembee katika nyayo za utawa kweli kweli. Simamisheni sala zenu tano kwa unyenyekevu. Na upole wa moyo kama ni wenye kumuona Mwenyezi Mungu. Na kamilisheni sawasawa saumu zenu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Na kila anayewajibika kutoa Zaka na atoe. Na mwenye faradhi juu yake kuhiji, wala hapana kinachomkataza, basi na ahiji kwenye Kaaba. Fanyeni wema kwa vizuri na acheni mabaya kwa kuyachukia. Jueni kwa yakini kuwa hakifai kabisa kitendo kisicho na utawa. Utawa ni shina la kila wema. Kitendo kisichopoteza shina hili hakitopotezwa. Ni wajibu kwenu kujaribiwa kama waaminio wa kwanza.

Kwa hiyo jitahadharini ili msiteleze. Ardhi haiwezi kuwadhuruni hata kidogo ikiwa mmefungamana sana na mbingu. Na kama ikiondolewa heshima yenu yote ya duniani Mungu Atawapeni heshima ya milele mbinguni, basi kwa hiyo msimwache kabisa. Hapana budi kuwa mtaudhiwa na mtaepushwa na matumaini mengi, basi msiyahuzunikie hayo kabisa. Kwani Bwana wenu Mungu Anawajaribuni ili Ajue kuwa mmekazania njia yake au hapana? Ikiwa mnapenda kusifiwa na malaika pia mbinguni, basi furahini mnapopigwa na shukuruni mnapotukanwa wala msikate kufungamana mnapoyakosa matumaini yenu kwa sababu ninyi ni katika Jumuiyya ya Mwisho ya Mwenyezi Mungu; basi onyesheni vitendo vyema vitakavyokuwa bora sana. Jueni kuwa katika ninyi kila atakayekuwa mvivu atatupwa nje ya Jamaat kama kitu kibaya na atakufa kwa huzuni wala hataweza kumdhuru Mungu chochote.

Tazameni mimi nawaambieni kwa furaha kubwa kuwa kweli Bwana wenu Mungu yupo! Na ingawa viumbe vyote ni viumbe vyake, lakini Mungu Anamchagua yule mwenye kumchagua Mungu. Na Anamkaribisha yule anayekwenda karibu yake. Na mwenye kumheshimu Naye pia Humpa heshima.

Njooni kwake Mwenyezi Mungu baada ya kunyoosha mioyo yenu na baada ya kutakasa ndimi zenu na macho yenu na masikio yenu. Na Yeye Atawakubalini. Ama kwa shauri la imani ya Mwenyezi Mungu; Anawatakeni mwamini kuwa Mungu ni mmoja na Muhammad, amani ya Mungu juu yake ni Mtume wake. Tena ni 'Khatamul-Anbiya' – Muhuri wa Manabii, na ni mbora kuliko wote. Wala hapana Nabii baada yake ila yule aliyevalishwa shuka la Muhammad, amani ya Mungu juu yake kwa njia ya mfano. Kwani mtumishi si mbali na bwana wake wala tawi haliko mbali na shina lake. Basi kwa hivyo mwenye kujitoa kwa kumfuata kweli kweli bwana wake anapata kwa Mungu jina la Nabii, na yeye havunji U-Khatamun-Nubuwwat. Kama vile mnapojitazama katika kioo hamuwezi kuwa wawili bali ni peke yako na ikionekana kwako wawili hapana tofauti baina yao ila tofauti ya kivuli na asili. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu Alivyotaka kwa Masihi Aliyeahidiwa. Na kwa ajili ya siri hii amesema Mtume Mtukufu, amani ya Mungu juu yake; "Masihi Aliyeahidiwa atazikwa katika kaburi langu, yaani yeyeni kama mimi wala hayakumtokea mabadiliko kinyume cha nilio nayo.

Tena jueni kwa yakini kuwa Isa mwana wa Mariamu amekwishafariki na kaburi lake lipo katika mtaa uitwao Khaniyar , katika Srinagar, Kashmir – bara Hindi. Na Mwenyezi Mungu Ameeleza kifo chake katika kitabu chake Kitukufu cha Kurani. Some aya hii; 'Falammaa tawaffaitaniy kunta antar –raqiba'alaihim' Basi uliponifisha wewe ukawa mlinzi wao . Na ikiwa maana yake aya hii ni nyingine, basi iwapi habari ya kufariki kwake katika Kurani Tukufu? Ikiwa aya zilizoonyesha kifo chake zina maana nyingine kama wanavyofahamu maadui zetu basi m aana yake Kurani haikutaja kifo chake pahali popote kwamba yeye atakufa au hafi? Ni ajabu Mwenyezi Mungu Ameeleza habari za kufariki kwake Mtume wetu Muhammd, amani ya Mungu juu yake, lakini katika Kurani nzima asieleze habari za kifo cha Nabii Isa bin Mariamu! Siri gani iliyomo ndani yake? Mkisema kuwa kifo cha Isa kimetajwa katika aya hii; "Falammaa tawaffaitaniy kunta antar-raqiba'alaihim" – Uliponifisha ukawa wewe ni minzi wao , aya hii inaonyesha kwa wazi wazi kuwa yeye amekufa kabla ya uharibifu wa Wakristo. Na kama maana ya aya hii ni kuwa Mungu Amemrufaisha Isa mbinguni mzima na kiwiliwili chake, basi kwa nini Mwenyezi Mungu hakutaja kifo cha mtu ambaye uzima wake umewaangamiza watu maelfu na maelfu? Na Mwenyezi Mungu amemweka mzima ili watu wawe mushrikina na wapotevu; ikiwa ni hivyo basi si makosa ya watu bali Mungu Mwenyewe ameyafanya ili awapoteze watu! Mkumbuke haiwezekani kuvunjika imani ya msalaba mpaka kihakikishwe kifo cha Masihi, mwana wa Mariamu.

Basi ni faida gani kudhania nabii Isa kuwa yu hai hilafu ya mafundisho ya Kurani Tukufu? Acheni afe ili dini hii ya Kiislam ihuishwe. Mwenyezi Mungu amedhihirisha kifo cha nabii Isa kwa kauli yake. Na Mtume, amani ya Mungu juu yake, amewona nabii Isa katika wafu usiku wa Miiraji. Pia bado hamjaamini? Imani hii ni imani gani? Je! Mnatanguliza masimulizi ya watu juu ya maneno ya Mungu? Dini hii ni dini gani ? Tena si kuwa Mtume wetu Muhammad, amani ya Mungu juu yake, ameshuhudia tu kwa kumwona nabii Isa katika wafu; bali amethubutisha kwa kufariki kwake mwenyewe kuwa hakuwa yeyote kabla yake aliyeishi milele. Basi maadui zetu kama wanavyoacha Kurani wanaacha Sunna vile vile; kwani mauti ni sunna ya Mtume wetu. Ikiwa nabii Isa yu hai basi kifo cha Mtume wetu ni fedheha kwake! Hakika ninyi hamuwi Ahlu Sunnat wala Ahlul Kurani mpaka mwamini kifo cha nabii Isa.

Na mimi sikatai utukufu wa nabii Isa. Ingawa nimeambiwa na Mwenyezi Mungu kuwa Masihi wa Muhammad, amani ya Mungu juu yake, ni bora kuliko Masihi wa Musa. Lakini pamoja na haya namheshimu sana Masihi bin Mariamu, kwani mimi ni Khatamul Khulafa wa Kiislamu kwa asili ya roho kama alivyokuwa Nabii Isa Khatamul Khulafa katika umati wa Israeli. Kama mimi nilivyo Masihi aliyeahidiwa katika umati wa Muhammad, amani ya Mungu juu yake, vivi hivi mwana wa Mariamu alikuwa Masihi aliyeahidiwa katika umati wa Musa. Kwa hivi mimi namheshimu yule aliye ni wa jina langu. Na ni mfisadi na mwongo anayesema kuwa simheshimu. Acheni Masihi hata ndugu zake wanne nawaheshimu kwa sababu wote watano walitoka tumbo m oja. Na zaidi ya haya nawaheshimu dada zake wawili kwa sababu hawa wote ni watakatifu wametoka katika tumbo la Mariamu bikira . Na utukufu wa Mariamu aliyejizuia nafsi yake wala hakuolewa mpaka muda mrefu, na baadaye kwa sababu ya kulazimishwa na wakubwa wa jamaa zake kwa ajili ya mimba akaolewa.

Kweli, ingawa, watu wanabishana kwa kusema kwa nini Mariamu kuolewa alipokuwa na mimba hilafu ya mafundisho ya Torati, na kuvunja ahadi ya ubikira, na kwa nini ikawekwa desturi ya kuoa zaidi ya mwanamke mmoja? Yaani ilipokuwa kwa Yusufu, Sermala, mkewe wa kwanza kwa nini Mariamu akakubali kuolewa na Yusufu. Lakini mimi nasema haya yote yalikuwa kwa shida iliyompata, na kwa hiyo anatakiwa kuhurumiwa sio kulaumiwa.

Baada ya maneno yote haya nasema mara nyingine, msidhani kuwa mmekiri dhahiri kwani kukiri dhahiri si kitu. Mwenyezi Mungu anatazama mioyo yenu na roho zenu, na atawatendeeni sawa na hali ya mioyo yenu.

Tazameni! Mimi natimiza faradhi ya kubashiri baada ya kusema haya kuwa; "Dhambi ni sumu msiile. Kumwasi Mwenyezi Mungu ni kifo kibaya kiogopeni. Ombeni ili mpewe nguvu. Sikilizeni, mtu asiyemfahamu Mwenyezi Mungu kuwa ana uwezo juu ya kila kitu wakati wa kuomba kwake hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyetanguliza dini, juu ya dunia, kweli kweli hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyeacha kila kitendo kibaya kama kunywa pombe na kucheza kamari na kutazama wanawake na kuzini na hiyana na rushwa, na kila jambo lisilojuzu kutenda na asiyetubia kutubu kwa kweli, hayumo katika jamaa yangu.

Mtu asiyedumu katika kusali sala tano siku zote hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyeshughulika katika kuomba kwa daima, wala hamkumbuki Mwenyezi Mungu siku zote kwa unyenyekevu hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyeacha rafiki mbaya mwenye kumwingiza mambo mabaya moyoni mwake hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyewaheshimu wazazi wake wala asiyezitii amri zao maarufu, zisizo kinyume cha Kurani Tukufu, wala hawatumikii kwa haki, hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyemfanyia wema mke wake na jamaa za mke wake kwa upole na ihsani hayumo katika jamaa yangu. Mtu mwenye kumnyima jirani yake hata kheri kidogo, hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyetaka kumsamehe mwenye kumkosea na mwenye kumbughudhi hayumo katika jamaa yangu. Kila mume mwenye kufanya hiyana kwa mke wake na kila mke mwenye kufanya hiyana kwa mume wake, hayumo katika jamaa yangu.

Mtu avunjaye ahadi aliyoahidi wakati wa kukiri na kuingia katika jamaa Ahmadiyya, kwa sababu yoyote, hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyeamini kwa kweli kuwa "mimi ni Masihi na Mahdi aliyeahidiwa", hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyejiweka tayari kunitii katika mambo maarufu, hayumo katika jamaa yangu. Mtu anayekaa pamoja na watu walionikataa na kukubali maneno yao ya upinzani hayumo katika jamaa yangu. Na kila mzinzi, fasiki, mlevi, mwuaji, mwizi, mcheza kamari, haini, mla rushwa, mnyang'anyi, mdhalimu, mwongo, mhadaa na mwenye kukaa na watu hawa wote, na mwenye kusingizia ndugu zake na dada zake na asiyeacha vitendo vyake vibaya, wala asiyeacha kukaa na watu wabaya, hayumo katika jamaa yangu.

Kumbukeni kuwa haya yote i sumu na baada ya kuzila sumu hizi hamuwezi kusalimika. Nuru na giza haiwezekani kukusanyika pahali pamoja. Kila mtu mwenye tabia yenye kujikunja wala si safi kwa Mwenyezi Mungu hawezi kupewa baraka inayopewa wenye mioyo safi. Bahati gani nzuri ya wale wanaosafisha mioyo yao na kutakasa roho zao na kila uchafu na kufungamana na Bwana wao Mwenyezi Mungu ahadi ya uaminifu! Hawatapotezwa kabisa!! Haiwezekani Mungu kuwafedhehesha sababu wao ni wa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni wa kwao. Nao wataepushwa na kila balaa. Ni mpumbavu adui yule ambaye awakusudia ubaya, kwa sababu wao wanabebwa na Mungu, yaani wamo katika ulinzi Wake.

Ni nani aliyemwamini Mwenyezi Mungu? Ni wale tu watakaokuwa kama hawa; Na vile vile ni mpumbavu yule anayefikiri kumtia udhia mtu mjeuri, mwenye dhambi, mbaya wa roho na mwenye nafsi ya shari; kwani yeye mwenyewe ataangamia. Tokea Mwenyezi Mungu kuumba mbingu na ardhi hata siku moja hajawaangamiza watu wema na kuwahilikisha au kuwafuta kabisa. Bali tangu zamani huonyesha ishara zake hata sasa. Yeye Mungu ni Mungu Mwaminifu na zinadhihirika ishara za ajabu kwa waaminifu wake. Watu wa dunia wanataka kuwaangamiza na kila adui anataka kuwahilikisha. Lakini aliye ni rafiki yao anawalinda katika kila pahali pa maangamizo na anawapa ustawi na ufaulu katika kila matokeo.

Bahati gani nzuri ya yule asiyeacha kamba ya Mwenyezi Mungu! Tumemwamini na tumemjua. Hakika Yeye ni Mungu wa walimwengu wote ambaye amenifunulia na ameonyesha kwa ajili yangu ishara zilizo kubwa, naye ndiye aliyenituma siku hizi niwe Masihi Aliyeahidiwa. Wala hapana Mungu mwingine ardhini wala mbinguni isipokuwa Yeye. Asiyemwamini amenyang'anywa bahati njema na ameshikwa na udhaifu. Tulipata ufunuo wa Bwana wetu Mwenyezi Mungu unaong'aa kama jua. Na tumeona ya kuwa Yeye ndiye Mungu wa dunia yote wala hapana Mungu mwingine ila Yeye tu. Nguvu zilioje za Yule tuliyemkuta na Mmiliki wa uwezo ulioje tuliyemwona! Kweli ni hii kuwa; hapana kitu kisichokuwa katika uwezo wake; ila kile kilicho khilafu ya Kitabu chake na khilafu ya ahadi Yake.

Safina ya Nuhu

Itaendelea toleo lijalo.

Jumuiya yazidi kubarikiwa na Allah

Kutoka uk. 2

iliyopita. Alipewa nakala ya 'Hekima ya mafundisho ya Uislamu' wakati wa Jalsa.

Alisema mara moja alipoanza kukisoma hakuweza kukiweka chini na kukaa hadi usiku wote alipokimaliza. Baada ya kumaliza kitabu alijisikia alikuwa amepata imani ya kweli. Alichukua Bai'at siku moja baada ya Jalsa.
Profesa wa chuo kikuu kutoka Japan alisema amekuwa akiitafiti Ahmadiya na pia amewahi kutembelea Rabwah. Wenyeji wake huko Rabwah walimuomba awasamehe kama kumekuwa na upungufu wowote katika ukarimu wao. Alisema alishuhudia mila hiyo hiyo iliyo bora ikijirudia katika Jalsa ya UK.

Mwanachama wa Bunge la Hispania alisema kwamba kwa kuona mipango ya Jalsa alihofia iwapo watu wa nchini kwake wanaweza kufanya kitu kama Jalsa kama wangetakiwa kuandaa kwa kiwango hiki. Baada ya tukio la siku tatu yeye alirudia kusema hakuna serikali duniani inayoweza kufanya kama vile wanavyofanya wahudumu wa Jalsa.

Mbunge mmoja mwanamke alisema Waahmadiya wanafanya kazi bila kuchoka kwa ajili ya kutafuta amani. Akizungumza katika mazingira ya kihistoria ya huko nyuma ya Waislamu kutawala Hispania alisema anatamani kumwambia Hazrat Khalifatul Masihi kuifikiria Hispania kama nyumbani kwake wakati atakapotembelea tena.

Familia kubwa ilikuwa imetoka Ufaransa ambapo wengi wao walishafanya Bai'at. Ingawaje baba yao, hakuwa amefanya Bai'at, lakini alivutiwa sana na sala ya Ijumaa na kusema amegundua baada ya kuja kwenye Jalsa kwa nini watoto wake waliikubali Ahmadiyya. Alisema aliwahi kupata ndoto katika ujana wake ambayo inawiana na aliyoyaona kwa kuhudhuria Jalsa kwa sababu ndoto ilikuwa juu ya kuwa katika mahali ambapo palikuwa na watu wengi waliokusanyika. Baba na mama wote wawili walichukua Bai'at wakati wa International Bai'at.

Mwanakundi wa ujumbe wa Kigiriki alisema hajawahi kuona taasisi nyingine yoyote ya Waislamu iliyo na mipango kama Ahmadiyya. Alisema kila mtu anamsalimia mwingine kwa upendo mkubwa katika Jalsa.

Mjumbe kutoka kundi wa washiriki wa Slovenia alisema kabla ya kuhudhuria Jalsa alikuwa akiifahamu Ahmadiyya kupitia maandishi tu, lakini sasa ameelewa kwamba kila alichokisoma kuhusu jamaat ni cha kweli kabisa, kwa mfano alijionea usemi wa Mapenzi kwa Wote Bila chuki kwa yeyote unavyotekelezwa kwa matendo. Profesa kutoka Chuo kikuu cha Slovenia alisema hii ni mara yake ya kwanza kuhuhduria shughuli yoyote ya kiislam, lakini amepata mtazamo chanya. Alivutiwa sana na moyo wa kujitolea ambao vijana waliokuwa wakigawa maji na chakula waliuonesha kwa wageni.

Afisa wa polisi kutoka Sweden alisema kuhudhuria Jalsa kulimpatia nafasi ya kujionea ujumbe wa Jumuiya ukiwekwa katika matendo. Alisema ujumbe wetu kama ungelifika Sweden yeye angeweza kustaafu kazi yake ya upolisi kwani hakutokuwa na haja tena ya polisi.

Mgeni kutoka Uswisi aliyekuja siku ya mwisho ya Jalsa alisema alishawahi kuona matukio mengi duniani kote lakini hajawahi kuona tukio kama Jalsa. Yeye aliona jinsi wahudumu walivyojitolea kwa upole bila kuonyesha hasira yoyote. Mgeni mwingine kutoka Uswisi alisema sehemu inayovutia zaidi ya Jalsa ilikuwa ni International Bai'at.

Mwandishi wa habari kutoka Jamaica alisema mpiga picha wake alikuwa na woga kabisa kuja katika mkutano wa Kiislamu. Mara tu Jalsa ilipoanza yeye alitilia shaka iwapo upendo unaoonyeshwa ulikuwa wa kweli au wa kujifanya tu. Katika hitimisho la Jalsa alisema hakuwa na shaka kwamba upendo na udugu wote ulikuwa halisi kabisa. Mwandishi wa habari huyo alimhoji Hazrat Khalifatul Masihi na kuahidi kujaribu kwa bidii ili kusambaza ujumbe wetu huko Jamaica.

Mgeni kutoka Panama alisema hajawahi kuona hali ya amani kama ya Jalsa mahali popote. Alishangazwa na yote aliyoyaona katika Jalsa na kusema sasa angeweza kikamilifu kuutetea Uislamu dhidi ya imani potofu.

Mgeni mwanamke kutoka Kazakhstan anasema ameshuhudia mengi ya dunia katika miaka yake 75 lakini aliona huduma ya kweli, na ubinadamu katika Jalsa. Alisema yeye alipata ubichi wa kiroho na nguvu baada ya Jalsa.

Mwanafunzi kutoka Guatemala alisema anga la kiroho la Jalsa lenyewe lilikuwa ni mwongozo.

Mbunge kutoka Croatia alisema huu ni uzoefu wake wa kwanza wa kuwa na Jumuiya ya Kiislamu. Alisema kama ujumbe wa amani alioutoa Hazrat Khalifatul Masihi kwenye hotuba yake ya ufungaji ungewekwa katika matendo basi dunia ingekuwa ni jukwaa la amani.

Mwandishi wa habari kutoka Sierra Leone alisema Jumuiya ilikuwa imemfanyia hisani kubwa kwa kumkaribisha kwenye Jalsa. Aliamua wakati Jalsa inaendelea kujiunga na Ahmadiya na alichukua Bai'at wakati wa International Bai'at.

Mgeni Ahmadia kutoka Ivory Coast alisema alikuwa Ahmadiyya kwa miaka mingi lakini hakuwahi kupata uzoefu wa kiroho hapo kabla kama alioupata kwenye Jalsa.

Mwanachama wa Chama cha Sanda ya Turin cha Uingereza alisema Jalsa ulikuwa ni mkutano bora kabisa kuliko mikutano yote aliyowahi kuhudhuria na kusema kuwa Jalsa ilimpa nafasi ya kujua mengi kuhusu Jumuiya.

Mtaalam wa Sanda ya Turin alisema moja ya malengo ya kuja Jalsa ilikuwa ni kuwafahamisha Waahmadiya kuhusu utafiti wake juu ya Sanda ya Turin lakini alijisikia kujifunza mengi zaidi kutoka Ahmadiyya.

Kwa neema ya Mungu Jalsa ilitangazwa sana kupitia vyombo vya habari na Idara ya vyombo vya habari.

Habari za Jalsa, picha za video, Televisheni na matangazo ya online yalifikisha habari kwa watu milioni 3.3. Watu milioni 2.79 walisikia kuhusu Jalsa kwenye redio ambapo watu milioni 7.7 walisoma kuhusu Jalsa kupitia magazeti. Vyombo vya habari vya kijamii vilifikisha ujumbe kwa watu milioni 5. Kwa jumla habari za Jalsa zimewafikia watu milioni 12.63.

Mbali na nchi za Afrika habari za Jalsa zilitangazwa katika televisheni nchini Uingereza, Scotland, Wales, Ireland, Marekani, Canada, Pakistan, India, Ufaransa, Jamaica, Bolivia, Ugiriki na Belize. Kituo cha televisheni kilichotoa habari zaidi ni BBC News 24 ambapo matangazo ya Jalsa yalirushwa mara tatu. Shirika la habari la Taifa la Kifaransa AFP pia lilitangaza kuhusu Jalsa na habari zilirushwa hewani kwenye mitandao mbalimbali ikiwa ni pamoja na Yahoo News, NBS News na MSN News. Jumla ya Radio 34 zilitangaza mahojiano ikiwa ni pamoja na BBC radio 4. Ambapo mahojiano ya dakika 20 yalirushwa.

Caroline Wyatt wa BBC alimhoji Hazrat Khalifatul Masihi. Catholic Herald lilichapisha makala ambapo makala mbili zilichapishwa katika Huffington Post. Ujumbe pia ulipelekwa kupitia Twitter. Haya yote ni matokeo ya kazi ya vyombo vya habari na timu kuu. Inaaminika kwamba Timu ya Waandishi wa Habari wa Jumuiya ya Uingereza pia ilifanya kazi katika kupeleka ujumbe kwa watu angalau milioni 2. Matangazo pia yalirushwa moja kwa moja kutoka Hadeeqatul Mahdi kwa ajili ya nchi zifuatazo za Afrika: Ghana, Nigeria, Sierra Leone, Uganda na Congo.

Msikilizaji mmoja kutoka Ghana alipiga simu na kusema yeye alikuwa Mkristo lakini alipata hisia za ajabu baada ya kuangalia Jalsa Salana moja kwa moja. Aliamini kwamba Jumuiya ya Ahmadiyya ilikuwa mstari wa mbele katika kuuwakilisha Uislamu. Alisema ni maombi yake atumie maisha yake yaliyobaki kama Mbashiri wa Jumuiya.
Mwanamke mmoja pia alipiga kutoka Ghana na kusema kuwa yeye ni Muislamu na baada ya kuona matangazo ya Jalsa yeye alitaka kuwa Ahmadia. Mtazamaji kutoka Uganda alisema alivutiwa sana na matangazo ya Jalsa kiasi kwamba alikwenda Msikiti wa Ahmadia na kuchukua Bai'at. Mtu mmoja pia alipiga simu kutoka Ghana na kusema Jumuiya inawakilisha Uislamu wa kweli. Lajna mmoja kutoka Ghana alipiga simu na akasema yeye alifurahishwa sana kuangalia MTA moja kwa moja akiwa ukumbini kwake.

TV ya taifa ya Sierra Leone pia ilirusha matangazo ya Jalsa Live. Mpiga simu aliwashukuru wale ambao kwa kazi yao aliweza kuangalia Jalsa na kumfanya ajisikie kama yeye yupo katika Jalsa. Matangazo ya Jalsa pia yalirushwa kwenye miji minne ya Congo. Huko Kinshasa idhaa ya TV ilikuwa imetenga masaa mawili tu ya matangazo lakini kwa vile hotuba ya mwisho ya Huzur ilipitiliza muda huo kituo hicho kilichukua hatua isiyokuwa ya kawaida ya kuongeza muda hadi hotuba ya Huzur kumaliza. Jambo hili lilipongezwa na wasikilizaji.

Watu wanaokisiwa milioni 10 walisikiliza matangazo ya Jalsa kwenye redio nchini Congo. Timu ya Vyombo vya habari na matangazo pamoja na timu ya MTA walifanya kazi vizuri sana hasa yule msimamizi wa matangazo yaliyoelekezwa Afrika. Kwa neema za Mwenyezi Mungu usambazaji wa matangazo ulikuwa mkubwa sana.

Namuomba Mungu Auongeze uwezo wa vijana kufanya kazi katika MTA na Timu ya Vyombo vya habari na matangazo.

Malalamiko yalipokelewa kwamba kulikuwa na ukosefu wa viti katika Ukumbi mkuu na baadhi ya wageni na wagonjwa hawa kupata viti kwa sababu baadhi ya vijana walikaa juu ya viti. Upangaji wa viti ni lazima uzingatie utolewaji wa beji za wanaokaa kwenye viti. Aidha nafasi zaidi kwa viti zinapaswa kutolewa au ukumbi tofauti unapaswa kuwa na utaratibu kwa wazee na walemavu. Ni lazima kuwe na screen zaidi ya moja.

Kwa ujumla hali ya vyoo ilikuwa vizuri ingawaje baadhi ya nyakati kulikuwa na malalamiko machache kuhusu ukosefu wa maji na karatasi za kujisafishia. Wageni wasio Wapakistan walilalamika kwamba wageni kutoka Pakistan hawakuonyesha uvumilivu kwenye maeneo ya bazaar (soko) ambako ilitakiwa kupanga foleni lakini wao hawakufanya hivyo na walikuwa wakiwasukuma watu wengine. Moja ya malengo ya Jalsa ni kuonyesha uvumilivu na kuvumiliana na kuwapa wengine haki zao. Mfumo wa usafiri kwa ujumla ulisifiwa lakini wafanyakazi walilalamika kuhusu tabia za baadhi ya wageni wachache.

Bila kujali ni nani, wageni ni wa familia ya watumishi wa ofisi za Jamaat au familia ya Hadhrat Khalifatul Masihi, ni wajibu wa kila mmoja kufanya kama wafanyakazi wanavyoelekeza. Vijana ambao walikuwa kazini wakanyongea na kusema afadhali wasifanye wajibu waliopangiwa kama watu hawawasikilizi. Hii pia si tabia sahihi. Wafanyakazi wanapaswa kuonyesha uvumilivu na kutoa taarifa kwa wakubwa wao ili kukabiliana na hali hiyo.

Kwa neema ya Allah Jalsa huleta baraka nyingi. Mwenyezi Mungu Ajaalie kila mtu ambaye alikuwepo katika Jalsa au aliyeangalia kwenye televisheni aweze kuleta mabadiliko ndani yake na Awajaalie wale ambao wamepata ujumbe kupitia vyombo vya habari wawe na hekima ili waweze kuelewa na kisha kukubali. Amin

Masjid Salaam, Shaaban Gonga na Maendeleo ya Kiswahili Tanzania

Na Mahmood Hamsin Mubiru,
Dar es Salaam

Kutoka toleo lililopita

Walipendana kiasi hiki ya kwamba Mwalimu Kiimbia aliposhambulia kitabu cha Sheikh Amri Abedi *'Sheria za kutunga mashairi na diwani ya Amri'*, Mohamed Ali alitoka na makala; *'Pole Mwalimu wa vijijini'*. Kwa muda wa miezi miwili mfululizo katika gazeti la 'Kiongozi' Mwalimu Kiimbia wa Kajunguti Bukoba alitoa makala *'Wataalamu msituharibie Kiswahili'* humo aliweza kutamka kwamba; 'Kiswahili si Kiarabu, na Kiarabu si Kiswahili'. Mohamed Ali alimshangaa mtalaamu huyo kutoka Kajunguti na akataka atoe jina la mtu yeyote aliyetoa madai hayo ambayo yalionesha bayana hayakuwa na figa wala chungu. Mohamed Ali pia alimwambia Mwalimu Kiimbia awe muangalifu jinsi anavyotumia maneno ya Kiswahili kwa mfano sio 'Nakala' bali ni 'Makala'. Neno Kadamnasi alikuwa amelitumia vibaya kwani alikuwa ameandika; 'Kumdhili mtu yeyote mbele ya kadamnasi ya watu'. Mohamed Ali alisema ilitosha kusema kumdhili kadamnasi. Mwalimu Kiimbia alimshambulia Sheikh Kaluta Amri Abedi bila kutaja jina kwamba maneno ya Kiarabu yanaingizwa katika Kiswahili; kwa mfano; 'Kaidahuna adhima', 'Waakhiri daawana', Mohamed Ali alisema hakuna neno lililokuwa limeingizwa katika Kiswahili ilikuwa ni destruri ya washairi kutumia maneno ya Kiarabu wakielewa kuwa wale waliokuwa wanawaandikia walikuwa wanaelewa. Bingwa Mohamed Ali alitoa mfano;

Wawapi maabidina, waabuduo jabari
Walo wakiswali suna, ntana na asifari
Qal –jara alayna, kalami makadir
Ayuhal maghruri, inahadaa dunia

Anatoa mfano mwingine;
Man Abul waladi, (nani baba wa mtoto huyu) hivyo akathibitisha ya kuwa ni desturi ya washairi toka zamani kuunganisha lugha mbili.

Mara ya pili kushika kalamu kumtetea rafiki yake ni wakati ilipotokea shairi la 'Raha' alilotunga Sheikh Kaluta Amri Abedi. Washairi wengi walikuwa na dhana potofu wakidhani Sheikh Amri alikuwa akimsema mtu mmoja aliyetuhumiwa kwa rushwa. Mohamed Ali kutokana na kufahamu khulka ya Sheikh Amri alisimama kidete na kupinga dhana hiyo kwa kusema;
Kwa ghafura mnang'aka, na mengi mno mafoko
Na masombo kujivika, majasho mtiririko
Silioni lilozuka, la kuwatia sumbuko
Dunia ni mzunguko, mtego umefyatuka

Kwa kasi mwavumburuka, na mingi misukosuko
Kwa maneno ya haraka, kweli mwaipiga mwiko
Huruma au wahaka, uliowatia shatiko
Dunia ni mzunguko, mtego umefyatuka.

Inabaki katika historia kuwa wakati Sheikh Amri Abedi anaumwa huko Ujerumani siku chache kabla hajafariki,

Masjid Salaam, Dar es Salaam: Makao Makuu ya Jamaat Ahmadiyya Tanzania

alimuandikia barua rafiki yake Mohamed Ali na katika barua hiyo akaweka ubeti ambao unafahamika kuwa ndio ubeti wa mwisho wa Sheikh Amri kabla hajafariki. Ubeti huo ni;
Nieleze yatukayo, majamo ya mtitimo
Yale yasisimuayo, kutamkwa na miyomo
Tutanabahi kwa hayo, tujiandae kwa fumo...

Pale Masjid Salaam palikuwepo na chuo cha kutayarisha wabashiri wa Islam kikiongozwa na Sheikh Kaluta Amri Abedi ambaye pia alikuwa ni mhariri wa gazeti la Mapenzi ya Mungu. Kama ilivyokuwa desturi kila asubuhi kijana alitumwa ili kuchukua barua kutoka posta. Moja ya barua hizo ilikuwa inakwenda kwa Mhariri wa Mapenzi ya Mungu. Aliisoma barua hiyo na kukuta shairi;
Mashairi ni adimu, yametutia kivuvu
Tupatayo ni adimu, twasoma kwa mazoevu
Kila aliyefahamu, asimame makamavu
Ghulamu mwinyi matano, tungo zino hatarini

Shairi hili lenye beti tisa linawaita akina Mwinyimatano, Salehe Bin Kibwana, Abdu bin Matunga, Abushiri wa Mbwana, Bin Waziri kijana, Mahmood Hamduni (Jitukali), Mathias Mnyampala, Sheikh Amri Abedi na Shaabani Robert waokoe sanaa ya ushairi kwani 'Tungo na utusi ndani' huitwa bidhaa mbovu.

Shairi hili lilimvutia sana Sheikh Amri hakuweza kukaa kitini bali alifunga safari hadi bandarini alikokuwa anafanya kazi Mwinyihatibu Mohamedi. Mtunzi huyo waliweza kuonana na Sheikh Amri alimpa hongera na akamkaribisha msikitini – Masjid Salaam. Na wakaahidiana pale walipokutana kusaidiana katika kuendeleza sanaa ya ushairi. Mwinyihatibu Mohamed akajenga desturi ya kutembelea msikiti wa Ahmadiyya na ndio maana katika magazeti ya Mapenzi ya Mungu ya zamani yapo mashairi mengi ya Mwinyihatibu Mohammed. Baadhi ya mashairi ya Mwinyihatibu Mohamed alimpatia Sheikh Amri Abedi ili aweze kuyahariri na jambo hilo linaelezwa vilivyo na Shihabuddin katika utangulizi wa *'Malenga wa Mrima'* anaeleza vizuri uhusiano wa Mwinyihatibu Mohammed na Sheikh Kaluta Amri Abedi.

Historia ya Ushairi inaonesha ni sheikh Kaluta Amri Abedi aliyeshughulikia utenzi wa 'Uhuru' uliotungwa na Mwinyihatibu Mohamed. Na ni kutokana na utenzi huo ndipo panapoibuka mjadala nani hasa aliyebuni neno 'Bunge'. Zipo rai tatu kuhusu neno hilo. Bwana Saidi Manoro Katibu Mkuu wa UKUTA anaeleza kwamba neno hilo sawa na maelezo yaliyotolewa na Mwalimu J. K. Nyerere katika mkutano wa kuzindua kitabu cha 'Mgeni Hassani' kiitwacho "*Rasil Ghuli*" katika ukumbi wa IFM Mwalimu Nyerere alisema; "Siku moja nikiwa ikulu alinijia mbio mbio Sheikh Amri na ni kwa sababu ninamjua siku n yingi nikamuuliza unanini Sheikh?" Sheikh Amri akamueleza Mwalimu kwamba amepata jina ambalo linaweza kutumika ili kueleza mahali wanapokutana wawakilishi wa watu ili kujadili maendeleo ya jamii. Sheikh Amri alisema ya kwamba amelipata neno hilo kutoka Buganda ambako mahali wanapokusanyika wawakilishi wa watu panaitwa Bulunge. Ni dhahiri ya kuwa ziko athari za Buganda katika maandishi ya Sheikh Amri Abedi. Ni kweli aliwahi kufanya kazi ya Ubashiri wa dini ya Islamu huko Uganda. Moja ya beti katika shairi lake linatoa ushahidi huo. Linasema;

Ima tawahesabia, waganda washusha chini
Wale zimewaparamia, motokaa za mijini
Hadi ukaja tambua, ushone za magotini
Nguo ziteremsheni, yapungue maasia

Hoja aliyoieleza Mshairi maarufu Shaaban Gonga inasema ya kwamba iliundwa kamati ya kushughulikia Lugha ya Kiswahili inasemekana katika Kamati hiyo alikuwepo Sheikh Shaaban Robert, Sheikh Mohammed Alli, Sheikh Abdulbari Diwani na Sheikh Kaluta Amri Abedi. Sheikh Shabani Gonga alieleza kuwa Sheikh Mohammed Alli ndiye aliyependekeza wazo hilo katika kamati hiyo neno hilo linatumika huko Mnyanyani – Tanga likiwa na maana ya kubungana (Kushauriana). Rai ya tatu imetolewa na Profesa Mugyabuso Mukokozi katika utangulizi wake wa Diwani ya Mwinyihatibu Mohammed iitwayo "*Malenga wa Mrima nimerudi*". Katika utangulizi huo Profesa Mulokozi anasema ya kwamba; "Mwinyihatibu Mohammed alisafirishwa na idara ya habari na utangazaji hadi Dar es salaam akamkabidhi rais – Mwalimu Julius K. Nyerere utenzi uitwao; *'Utenzi wa Uhuru wa Tanganyika'*. Ndani ya utenzi huo ndimo marehemu Amri Abedi aliyekuwa Waziri wa Utamaduni alimolitoa neno 'Bunge' na kutoka hapo likaanza kutumika na kukubaliwa na rais wa nchi. Na kabla ya hapo inasemekana ya kuwa neno hilo lilikuwa halijawahi kutumika.

Maelezo yote yaliyotolewa inaonekana ya kuwa yakawa na mashiko. La msingi hapa ni kwamba ukarabati wa mwisho wa neno hilo ulifanywa na Sheikh Kaluta Amri Abedi. Upo uwezekano huko Uganda aliona neno Bulunge na kutoka kwa Mohammed Alli alipata neno kubungana ambalo pia amelitumia. Ustadhi Mwinyihatibu Mohammed katika utenzi wa Uhuru amelitumia neno hilo ni vigumu pia kumaizi kwamba neno hilo hatimaye alilitohoa Sheikh Kaluta Amri Abedi, kwani hatuna ushahidi wa mahali popote alipoandika kwamba yeye ndiye aliyetunga neno hilo.

Ikumbukwe ya kwamba si lazima kubuni neno au kuliunganisha wewe, bali hoja ya msingi hapa ni kuwa ni nani hasa aliyelileta neno hilo kwenye utamaduni wa jamii husika. Kwa mfano neno Ikulu ambalo hutumika kueleza mahali anapoishi Rais na makao makuu ya serikali ni neno ambalo Sheikh Amri alilitoa katika utamaduni wa jamii nyingi za Tanzania ambazo mahala alipokuwa anaishi Mtemi palikuwa panaitwa Ikulu.

Licha ya kuwa mshairi maarufu Shaabani Gonga kama alivyokuwa Sheikh Kaluta Amri Abedi alikuwa na sifa mbili za kuwa Mshairi na Mwanasiasa. Ni katika harakati za siasa alipoweza kukutana na Saadan Abdulkandoro. Ikumbukwe kwamba Sheikh Kaluta Amri Abedi aliwahi kuwa Katibu wa TAA wa Dar es salaam na ni hapo katika msikiti wa Masjid Salaam ndipo Shaabani Gonga alipokutana na mpwae Sheikh Kaluta Amri Abedi yaani Saadani Abdulkandoro. Kujuana huku kuliongeza hamasa ya kisiasa na kuendeleza lugha ya Kiswahili. Saadani Abdulkandoro alitumia vilivyo sanaa ya Ushairi katika kuhamasisha ukombozi wa Tanzania. Saadani aliendelea kumueleza Sheikh Amri aliyekuwa masomoni Rabwah – Pakistani mapambano ya uhuru yaliyokuwa yanaendelea huku Tanganyika. Moja ya beti aliyomtumia ni hii ifuatayo:-

Nyoka amegutuka, ndani ya shimo kutuna
Tena amekasirika, hasira zenye kunena
Nyoka anababaika, shimoni kwa kujikuna

Endelea uk. 7

Bustani ya Washairi

NAHUBIRI KUWA AHMAD, NAYE NI RASULI

Nahubiri kuwa Ahmadi, Naye ni Rasuli
Ametumwa na Mola Wadudi, si mwongo asili
Na ukweli mno twaunadi, tulimkubali
Kila mbinu tunajitahidi, kuwa wahubiri

Bali wengi bado wakaidi, kwa huo ukweli
Kila siku viburi mwazidi, hamutafakari
Abadani nyuma hamrudi, mumejivinjari
Mwamtenda mwingi ufisadi, na kumuadhiri

Mwamtenda mwingi, ufisadi na kumkejeli
Munasema yeye Ahmadi, eti ni kafiri
Mwapingana na Mola Wadudi, dhahiri shahiri
Maskini munajihusudi, mnajikatili

Enyi watu mnajihusudi, ninawahubiri
Maana mnomkaidi, msomkubali
Ndiye Issa muelewe hadi, wa mara ya pili
Nabii wetu hasa Muhammad, alomtabiri

Ndiye huyu muelewe hadi, Ameshwasili
Kesha tumwa na Mola Wadudi, wazi na dhahiri
Nawambia enyi wakaidi, muijuwe siri
Ndiye huyo Imamu Mahdi, tunomsubiri.

Ndiye huyo Imamu Mahdi, Ameshadhihiri
Kesha fika kulianza kundi, lile lenye kheri
Kwenye dini ya Mola Wadudi, liso na batili
Muhammad alilolinadi, pekee halali

Narudia enyi wakaidi, ninawahubiri
Ni nabii nae Ahmadi, katu si kafiri
Nawambia ila makusudi, mulitafakari
Musimwasi mpendwa Wadudi, na mtahadhari.

Nahubiri enyi wakaidi, mtafakari
Ni Nabii naye Ahmadi, mtahadhari
Mtajibu nini kwa Wadudi, Msokubali
Na ujumbe kutwa twaunadi, mwaukejeli

Mutajibu nini kwa Wadudi, Msokubali
Na ujumbe kutwa twaunadi, twauhubiri
Bali ninyi munajitahidi, kuubadili
Ili haki ionekwe hadi, ndio batili

Mutasema nini kwa Wadudi, siku ya kikiri
Nawambia enyi wakaidi, Wenye viburi
Ni nabii naye Ahmadi, Musomkubali
Mtasema nini kwa Wadudi, Mtahadhari.

Bimkubwa Kombo, Zanzibar.

HAKIKA NI MAAJABU

Kwa jina lake Rabbana, kalamu naicharaza,
Japo si mjuzi sana, lakini kheri kupwaza,
Mengi niliyoyaona, ukweli yanashangaza,
Hakika ni muujiza, hii Jalsa Salana.

Wasomaji waungwana, naanza kuwaeleza,
Upendo kushikamana, hakuna anojikweza,
Watu wametulizana, pasina fujo kuzoza,
Hakika ni muujiza, hii Jalsa Salana.

Salam alekum sana, kila mmoja apaza,
Ukitafakari sana, kipo cha kujiuliza,
Huu simfano wa janna, Qurani imeeleza,
Hakika ni muujiza, hii Jalsa Salana.

Hutuba kusomeana, watu wanasikiliza,
Usiku kucha mchana, ni mambo ya kupendeza,
Ikinadiwa adhana, hakuna mwana kucheza,
Hakika ni muujiza, hii Jalsa Salana.

Ishara zaonekana, kidogo tu ukiwaza,
Ni nuru ya Maulana, ndio inayo angaza,
Kila unae muona, rohoye kanyenyekeza,
Hakika ni muujiza, hii Jalsa Salana.

Viongozi wakinena, hakuna mwenye kubeza,
Utii utauona, wote wanatekeleza,
Na nidhamu kila kona, hakika wamejaliza,
Hakika ni muujiza, hii Jalsa Salana.

Maradhi moyo hupona, hata kama ulioza,
Dunia sio maana, mengi ni mauzauza,
Usiposhiriki bwana, ni rahisi kupooza,
Hakika ni muujiza, hii Jalsa Salana.

Tuombe kwa Subhana, Atujaie uweza,
Tufanye juhudi sana, mia mia kuwekeza,
Kila mwaka kuonana, Mola Atatuongoza,
Hakika ni muujiza, hii Jalsa Salana.

Hakuna chakubishana, hapa ninaishiliza,
Mengi yanaonekana, machache nimeeleza,
Msiopanda safina, chonde Jalsa chunguza,
Hakika ni muujiza, hii Jalsa Salana.

Mwl. Najat Fakim Saidi, Marungu, Tanga.

IPUA

Bismillahi stata, dua ninayoanzia,
Kalamu nimekamata, swahiba nakuusia,
Chungu kinapofukuta, ni maji uliyatia,
Ip! ip! we ipua, chungu kimeshatokota.

Jiko zuri umepata, mbona unaliachia,
E bwana acha kusita, hebu kwanza fikiria,
Utakayo ni matata, ina machungu dunia,
Ip! ip! we ipua, chungu kimeshatokota.

Jiko zuri umepata, ni safi kwa kupikia,
Wali viazi mbatata, kwa raha utajilia,
Baridi ikipuputa, maji wajichemshia,
Ip! ip! we ipua, chungu kimeshatokota.

Miaka mingi yapita, bado lakusubiria,
Kila unapolikuta, la moto limekolea,
Ni heri tu kulivuta, nyumbani kujiwekea,
Ip! ip! we ipua, chungu kimeshatokota.

Bahati umeipata, na sasa waikimbia,
Ndoto ulizoziota, zote zimeshatimia,
Unapoziba ukuta, utakuja kujutia,
Ip! ip! we ipua, chungu kimeshatokota.

Hasara itakukuta, majiko ya kufutia,
Hakijaiva wachota, mbichi wajitafunia,
Tumbo litaposokota, mi simo nishakwambia,
Ip! ip! we ipua, chungu kimeshatokota.

Wino unakatakata, hapa ninamalizia,
Utapokuja kufyata, somo nakuhurumia,
Wengine wakilipata, na watajifaidia,
Ip! ip! we ipua, chungu kimeshatokota.

Mwl. Najat Fakim Saidi, Marungu, Tanga.

NALIA DUNIA YANGU

Kwa jina lake Rabana, nashika kalamu yangu,
Kwa wazee na vijana, zisomeni beti zangu,
Na mtafakari sana, jamani chonde wenzangu,
Nalia dunia yangu, ina mtihani sana.

Kusudi la Maulana, kunipa uhai wangu,
Ni kumuabudu sana, niwe na sifa za Mungu,
Ila ni kinyume bwana, hadi naona uchungu,
Nalia dunia yangu, ina mtihani sana.

Ona maajabu ona, naficha vitendo vyangu,
Simwogopi Subhana, naogopa walimwengu,
Damu yangu naikana, uko wapi utu wangu,
Nalia dunia yangu, ina mtihani sana.

Mwandani na wangu wana, kwao ni kizunguzungu,
Shida zimezidiana, halikidhi langu fungu,
Kila siku ni hakuna, hadi chawa kutu chungu,
Nalia dunia yangu, ina mtihani sana.

Na maradhi sijapona, yatele moyoni mwangu,
Naweka wazi bayana, si shwari nyumbani kwangu,
Machungu ninayoona, ni heri upigwe rungu,
Nalia dunia yangu, ina mtihani sana.

Umezidi ujana, hadi zatetema mbingu,
Ni balaa kila kona, ukitaja jina langu,
Nguo zangu za kubana, eti naiga uzungu,
Nalia dunia yangu, ina mtihani sana.

Kiburi si maungwana, sababu ya cheo changu,
Yani napenda ubwana, niwe mithili ya mungu,
Kumbe chochote hakuna, ila najivisha pingu,
Nalia dunia yangu, ina mtihani sana.

Dua zenu waungwana, hiki cha mwisho kifungu,
Nahitaji mi kupona, na mimi ni mche Mungu,
Dunia ina fitina, Mola nitoe ukungu,
Nalia dunia yangu, ina mtihani sana.

Mwl. Najat Fakim Saidi, Mtiti, Tanga.

KATUKIRIMU RABUKA, YETU JALSA SALANA

Kwa jinale Maulana, kalamu naiandama
Naandika kwa mwanana, yetu Jalsa Salana
Qadiri yake Rabana, kwa wana na awalina
Katukirimu Rabuka, kwayo Jalsa Salana

Kikao cha Utukufu, kakianzisha Masiha
Nabii wetu adhimu, kwa kizazi akheria
Huondoa kila sumu, kwa mwenye kushadidia
Katukirimu Rabuka, kwayo Jalsa Salana

Kusanyiko lenye shani, ikighaniwa Qurani
Wana huzinanga nyingi, sifa kadha za Jalali
Hawaachi kubashiri, ubora wa Muhammadi
Katukirimu Rabuka, kwayo Jalsa Salana

Hii Jalsa Salana, Mkutano wenye sifa
Tangu pale Qadiana, Hata kule Amerika
Gayana, Kenya na Ghana, Jalsa hupata shika
Katukirimu Rabuka, kwayo Jalsa Salana

Jalsa tunayosema, si jambo la lelemama
Wachamungu hukutna, kwa huba hata bashasha
Jambo lao la amana, kusabihi Maulana
Katukirimu Rabuka, kwayo Jalsa Salana

Umoja wa Maulana, huwa tambio la sana
Wana husameheana, yalowasibu kwa mwaka,
Hujuliana jamaa, tawi hata na majina
Katukirimu Rabuka, kwayo Jalsa Salana

Ukhalifa ndio ngao, ya Jalsa Salana
Wana hutweta kwa semo, wakiunadia umma
Thamani ya kamba yao, ilo toka kwa Muumba
Katukirimu Rabuka, kwayo Jalsa Salana

Wana hujifunza vema, wakiwa kwenye Jalsa
Kumkurubia Bwana, kujitolea mtima
Kuzihifadhi amana, kukumbatia yatima
Katukirimu Rabuka, kwayo Jalsa Salana

Wajibu wa kila mja, alofika hadharani
Kutanabahisha umma, Ayapendayo Manani
Tena kaenda mrama, Asohubiri amani
Katukirimu Rabuka, kwayo Jalsa Salana

Rabbi Ewe Mtajika, twakushukuru hakika
Kutuletea fadhila, Baraka za Ukhalifa
Umetupa hila pana, kututunuku Jalsa
Katukirimu Rabuka, kwayo Jalsa Salana

Ya Rabbi swali Karima, Umpe nyingi salamu
Muhammad Muadhama, mbora wa wanadamu
Mwanae pia adhima, Masiha wa zama zetu
Katukirimu Rabuka, kwayo Jalsa Salana

Kwa heri ndugu kwaheri, kwa heri ya kuonana
Tumejifunza mazuri, kwenye Jalsa Salana
Pasi na budi kukiri, tutekeleze kwa mana
Katukirimu Rabuka, kwayo Jalsa Salana

Seif Hassan Nakuchima, Dar es Salaam

Al Ustadh Khamis Wamwera akumbuka

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

Jina langu ni Khamisi Sultan Shamte Koingato Nnyeme Wamwera. Nimezaliwa yaumulkhamis ya tarehe 13 April, 1938 katika kijiji cha Nyipara tarafa ya Rusende wilayani Rufiji. Masomo yangu ya shule nilianza mwaka 1950 hadi mwaka 1957 nilipokhitimisha kwa kupata elimu ya darasa la nane.

Nimejiunga katika Jumuiya ya Ahmadiyya mnamo mwaka 1955 mara tu sheikh Swaleh Mbaruku Kapilima alipowasili kijijini kwetu. Nilikuwa mmoja miongoni mwa vijana wachache waliokuwa wameathirika na maelezo yaliyotolewa juu ya maswala mbalimbali ya Islam. Baba yangu mzazi hakuwa mwepesi kukubali ukweli wa kuendelea utume, kifo cha nabii Isa a.s. na ufikaji wa Seyidna Ahmad a.s. katika zama hizi. Bali baba mdogo baada ya muda alifanya baiati na kujiunga katika Ahmadiyya. Kisha baadaye, baada ya miaka kadha kupita, baba mzazi naye akajiunga katika jamaat.

Mwaka 1956 mjini Dar es salaam ulijengwa na ukafunguliwa msikiti ambao hadi sasa tunao tunaendelea kuutumia. Pamoja na msikiti huu, pia palifunguliwa chuo cha wabashiri kilichojulikana kwa jina la Ahmadiyya Muslim Missionary College kikiongozwa na sheikh Kaluta Amri Abeid. Mimi nilijiunga na chuo hiki mwaka 1958 nikiwa na ndugu yangu mpenzi mwalimu Omari Abdullah Matimbwa kutoka Rufiji. Tulikuwa vijana 15 kutoka sehemu mbalimbali ya Tanganyika kwa wakati huo. Sisi tulikuwa kundi la pili baada ya kundi la kwanza la akina mzee Mbwana Shamte Nyengo na Juma Abdullah Mpitakunza kumaliza muda wao.

Zilikuwa siku za vuguvugu kubwa la siasa. Ni wakati wa harakati za kudai uhuru wa Tanganyika. Waislamu pia tulitakiwa kuwamo katika msafara huu. Maulana Sheikh Mubarak Ahmad H.A. akiwa Mbashiri Mkuu Afrika Mashariki aliwahamasisha Waislamu na kuwahimiza Waahmadiyya wananchi kutobaki nyuma kwenye uwanja wa mchezo wa siasa. Alimwombea ruhusa sheikh Amri Abedi Kaluta kwa Khalifa mtukufu wa Pili wa Seyidna Ahmad a.s. ili aingie kwenye kilinge cha siasa. Khalifa mtukufu alikubali ombi hilo na sheikh Amri akaingia siasani. Alibaki kuwa mtu wa dini pia mwana siasa. Naam alikuwa mtu wa kutegemewa mno kwenye kilio cha kudai uhuru akishirikiana na mwalimu Julius Nyerere na wengineo.

Pamoja na hayo bado tuliendelea kuchota elimu ya dini chini ya uongozi wa sheikh Amri hadi mwaka 1960 alipochaguliwa kuwa Meya wa kwanza mwafrika kushika wadhifa huo katika jiji la Dar es salaam. Mabadiliko ya uongozi wa Jamaat pia yalipatikana. Aliletwa maulana sheikh Muhammad Munawwar kutoka Nairobi Kenya kushika nafasi ya sheikh Amri ambaye sasa alikwisha ingia katika uwanja wa siasa. Naam, masomo yetu yaliishia mwaka 1962. Mimi niliteuliwa kwa kazi za ofisini nikimasaidia sheikh Munawwar. Wenzangu walitawanywa sehemu mbalimbali ya nchi yetu tayari kwa ubashiri.

Sasa tunaye maulana sheikh Muhammad Munawwar H.A. binafsi nimefanya naye kazi takriban miaka kumi hivi. Nilimfahamu vyema. Kwa umbile, hakuwa mwembamba, bali hakuwa mrefu wa kuchusha. Alikuwa mhindi kwa taifa, bali alijazwa na khulka na mafundisho ya kiislamu. Alikuwa mkakamavu alikuwa akitazama mbele aendako. Alipenda kutembea kwa miguu. Alikuwa mvaaji wa mapajama, mateitei na yale mashati marefu. Kichwa kilikuwa kikipambwa na kilemba cheupe na mkononi mli na aswaa aliyonyooka.

Maulana sheikh Muhammad Munawwar ni mchapa kazi makini sana. Alikuwa anapenda mno kusoma vitabu na magazeti mbalimbali, yawe ya dini au ya dunia. Alikuwa mzungumzaji fasaha wa Kiswahili nami sikuona vibaya kujifunza lugha hii kutoka kwake. Kauli yake ilikuwa haina tenge. Ndivyo alivyokuwa anastaajabisha watu alipokuwa anasema kijaluo lugha mojawapo ya makabila makubwa ya Kenya.

Maulana sheikh Muhammad Munawwar H.A. aliteuliwa kuwa mbashiri mkuu mara tu nchi hizi tatu zilipopata uhuru kwa miaka tofauti. Sheikh Munawwar alikuwa mbashiri mkuu Tanganyika. Uzito wa kazi kwake uliongezeka mara dufu. Alikuwa mhodari wa kazi. Alikuwa mvumilivu, mwenye maneno laini na wakati mwingine alitoa maneno ya utani. Mara zote sheikh alikuwa mwenye wajihi wa furaha na bashasha. Lakini alikuwa anabadilika ghafla hasa anapoona au kukutana na maneno ya kuikashifu dini ya kiislamu au maelezo ya kuvunja heshima ya mtukufu mtume Muhammad s.a.w. Alikuwa mkali kwelikweli alipokuwa akiona maandiko ya kumdhalilisha seyidna Ahmad a.s. sura yake hubadilika na ile bashasha hutoweka. Hatulii aslani mpaka atowe jibu la tuhuma hizo zilizorundikwa juu

Maulana Sheikh Mubarak Ahmad H.A. Aliyekuwa Mbashiri Mkuu wa kwanza Afrika Mashariki

ya Islam na viongozi wake. Wallahi nakwambia alikuwa haondoki mezani hadi anahakikisha majibu yamepatikana. Kazi hii alikuwa anaifanya hadi usiku wa manane ambapo aliacha ofisi na kwenda kwenye sala ya tahajjud. Asubuhi majibu ya wapinzani yalikuwa tayari yamepatikana kwa njia ya VIKARATASI! Mara nyingi mtihani huu mimi nilianguka. Mimi nilikuwa naye hadi wakati fulani tu baadaye nilikwenda kulala nikimwacha ofisini akiendelea na kazi peke yake.

Katika ibada, sheikh Muhammad Munawwar alikuwa mafano mwema. Mara nyingi alikuwa anafunga saumu za nafali na alikuwa anatowa sadaka za namna namna. Wakati wa sala alikuwa anauheshimu sana. Ule wakati ambao tulikubaliana ukifika, basi sala ilisimama. Na sala ya tahajjud kwake ilikuwa kama ya faradhi. Katika mwezi mtukufu wa Ramadhani ndiyo kabisa alikuwa anaongeza nguvu ya ibada zake. Naye alikuwa anatuhimiza sana kumwomba na kumtegemea Mwenyezi Mungu. Alikuwa anatuhimiza tumwombe Mungu ili watu wa nchi hii waikubali dini ya Islam na bendera yake ipepee kote duniani. Ukweli wa Seyidna Ahmad ufahamike na wengi wao wajiunge katika Ahmadiyya.

Wakati fulani nakumbuka Sheikh Muhammad Munawwar alituambia ya kwamba utafika wakati watu wengi watajiunga katika jamaat. Khofu na wasiwasi iliyokuwa imetanda kuwa ukijiunga katika Ahmadiyya utazikwa na nani itaisha. Sheikh alitudokeza tusiwe na wasiwasi hali ya Jumuiya itakuwa nzuri mambo yatabadilika. "Leo (kwa wakati huo alisema sheikh Munawwar) msikiti huu, masjid Salaam haujazi wanajumuiya hata mstari mmoja tunaposwali, lakini juweni wakati utafika msikiti huu utajaza na utaonekana mdogo". Maneno haya alitamka sheikh Muhammad Munawwar miaka 35 iliyopita. Wakati maneno haya yalipotamkwa yalionekana vichekesho. Lakini sasa maneno hayo yananihakikishia kinywani mwa mtu wa Mungu. Hapana shaka alikuwa mcha Mungu na mtawa. Sikujaaliwa kuandika kila khutuwa. Lakini nimalizie kwa kusema tu kwamba sheikh Muhammad Munawwwar alikuwa mtu wa huruma. Vijana kadhaa walisomeshwa naye kwa kutoa karo za shule hadi kufikia sekondari na wengine vyuo vikuu.

Alikuwa mume wa wake wawili ambao walikuwa wanafika hapa kwa zamu. Bali nyumbani mwake hapakuwapo makubwa. Chakula chake kikubwa sana kilikuwa chapati na nyama ya kima, mbogamboga na dengu. Walikuwepo wengine wengi wa kumsaidia kazi wakati wakeze hawapo naye, aliishia kumshukuru tu na kusema "Jazakumullah" na shughuli kuendelea kuifanya yeye mwenyewe.

Masjid Salaam, Shaaban Gonga

Kutoka uk. 5

Siafu wanakazana, nyoka amekasirika

Saadani alikuwa na uhusiano pia na Mshairi mwingine maarufu wa Ujiji Kilume Ahmad (Snow white – Akilimali). Snow white alijuana na Sheikh Amri wakati wote wakiishi Tabora na wakiwa Tabora huko aliweza kumwandikia utangulizi wa Diwani yake iitwayo; "*Diwani ya Akilimali*". Katika utangulizi huo Akilimali anatoa shu Qur'ani na anasema;

"Namshukuru sana Sheikh Kaluta Amri Abedi wa Ahmadiyya Muslim Mission aliyenisaidia kukisahihisha kitabu hiki na kuandika dibaji fupi ya kitabu hiki. Kazi nzito na ya sifa imefanywa na Sheikh huyu. Maneno haya yanatukumbusha kitabu maarufu cha Ernest Heming way 'A Movable Feast'. Kama ilivyokuwa katika kitabu hicho cha Ernest Heming way 'A Movable Feast' nyumba ya Shabaani Gonga iliwaleta pamoja washairi maarufu wa nchi hii. Na ni kweli ilikuwa ni tafrija kubwa nyumbani kwa Shabaani Gonga ambapo Sheikh Amri Abedi hakukosa na washairi wengine maarufu wa Tanzania walitembelea sana hapo. Wakiwepo akina Abu Saidi, Saidi Makarani, Juma Mohammed (Mtu kitu), Mohammed saidi (Mtu chake), Sihiyana Swaleh Mandevu (Mtenda mema), Abdu Nasibu (jicho), Swaleh Kibwana (kunguru mwoga), Palamlanzi Hassani ingawaje yeye ni mwenyeji wa Rufiji muda wake mwingi alikuwa mjini Dar es salaam kwa sababu alikuwa akifanya kazi 'New African Hotel'. Wakati Shaabani Gonga alikuwa akifanya kazi benki 'Barclays Bank' na hapo waliweza kukutana na wakabadilishana mawazo na kuweza kuelezana mikakati ya kuweza kuendeleza ushairi.

Wakati nikiendelea na utafiti wa makala haya alibisha hodi nyumbani kwa Shaabani Gonga Bw. Adam Nanjase mshairi mwenye kumbukumbu ya ajabu. Mashairi mengi maarufu ya zamani ameyahifadhi kichwani. Alikuwa amekuja pale kwa Shaaban Gonga ili kumjulia hali. Na kwa mara ya pili nilikutana na Bw. Adam Nanjase kwa Amir Sudi Andanenga ambaye wana uhusiano wa damu. Ni burudani ya kukata na shoka Amir Sudi Andanenga na Adam Nanjase wanapokutana. Mmoja akianza shairi mwingine anamalizia. Kwa mfano shairi la kuchuma najitahidi sina bahati mwenzenu la Idi Saidi Moyoladi Adam Nanjase alipoanza kulighani Amir Sudi Andanenga akamalizia.

Kuna somo kubwa katika maisha ya Shaabani Gonga. Huyu ni mshairi ambaye amefanya bidii kubwa ya kujiongezea elimu. Ni mshairi ambaye anapenda saana kufanya utafiti na mwenye kumbukumbu. Utafiti mkubwa alioufanya ni kuandika juu ya maisha ya Mathias Mnyampala, Khamisi Amani Khamisi Nyamaume na Mahmood Hamduni (Jitukali). Ni dhahiri ya kwamba Shaabani Gonga amekwishatoa Diwani ya mashairi ya Hamisi Amani Hamisi Nyamaume, diwani hiyo inaitwa 'Diwani ya Nyamaume'. Na tayari alikwisha kusanya mashairi ya Jitukali na alikuwa na mipango ya kuyachapisha mashairi hayo. Ni jambo la kufurahisha kuelewa ya kwamba uchunguzi huo wa Shaban Gonga na washairi hao umewaleta karibu washairi hao na kuwafanya ndugu. Urafiki huo unaendelea kwenye familia zao

بسم الله الرحمن الرحيم

JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA TANZANIA - KALENDA YA MATUKIO KWA MWAKA 2015/2016

MWEZI	MWAKA	TAREHE	TUKIO
JULAI	2015	01 – 10	Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa – Dar es Salaam.
		10 – 17	Siku maalum za kukutana na viongozi wa serikali/waandishi wa habari sehemu walipo kwa lengo la kuleta uhusiano nzuri.
		17	**Sikukuu ya Eid Ul Fitri***
		17 – 24	Siku maalum za makusanyo ya michango ya Waqf-e-Jadid na Tahrik Jadid
AGOSTI	2015	1 – 8	Maonyesho ya Kilimo kitaifa - Mikoa husika
		21 – 23	**Jalsa Salana Uingereza**
SEPTEMBA	2015	1 – 10	Siku maalum za maonyesho ya vitabu katika Mikoa husika.
		07 – 14	Wiki maalum ya kuchanga mchango wa mkutano wa mwaka (Jalsa Salana)
		19 – 20	Uendeshaji wa semina za Tabligh katika kila tawi.
		24	**Eid Ul Adhha***
OKTOBA	2015	2-4	**Jalsa Salana Tanzania**
		24	Siku ya mwisho ya kupokea ripoti za makusanyo ya Tahrik Jadid 2014/15
NOVEMBA	2015	7-8	**Siku maalum za mahubiri nchi nzima.** Mahubiri yafanyike, viongozi wote wa Matawi ni lazima washiriki, ripoti itumwe Makao Makuu.
		15 – 29	Ahadi za Tahrik-e-Jadid kwa mwaka mpya (Novemba 2015 / Oktoba 2016)
		22	**Siku ya waanzilishi wa dini.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii hii).
		27	Mitihani kutoka kitabu cha: **Zawadi kwa Kaisari**
DISEMBA	2015	01 – 15	Siku maalum za kukusanya malimbikizo ya Waqf-e-Jadid.
		12 – 13	Ijtimaa ya Ansarullah Kitaifa - Dar es Salaam
		25 – 31	Siku maalum za Tarbiyyat Kitaifa. (Msukumo uwekwe zaidi kwa Waahmadiyya wapya).
		20	**Siku ya Seeratu Nabii.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii).
JANUARI	2016	11 – 18	Ahadi mpya za Waqf-e-Jadid kwa mwaka 2016.
		22	Mitihani kutoka Kitabu cha: **Ushindi wa Islam**
		24 – 31	Siku maalum za makusanyo ya mchango wa kawaida.
FEBRUARI	2016	01 – 06	Siku maalum za kuwaalika wageni kwa mazungumzo katika Jamaat zote. Taarifa zitumwe Makao Makuu.
		20	**Siku ya Mwana Aliyeahidiwa.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii).
		26 – 28	Siku maalum za kuwatembelea wagonjwa, mahospitalini na majumbani. Pia kuwatembelea mayatima, walemavu, na vikongwe (washiriki, Ansar, Khuddam na Lajna).
MACHI	2016	01 – 09	Siku maalum za kufanya vikao vya kujadiliana ajenda za Shura ya 2016 na kuchagua wajumbe.
		12 – 13	Mahubiri Maalum kwa kila tawi. (Viongozi wote ni lazima washiriki).
		18	Mahubiri ya tarehe 12 – 13 yatolewe maelezo yake mbele ya Wanajumuiya wote.
		23	**Siku ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii).
		31	Siku ya mwisho ya kutuma dondoo za Mushawara kutoka matawini kwa ajili ya Shura ya mwaka 2016.
APRILI	2016	08	Mitihani kutoka kitabu cha: **Nyota ya Kaisari**
		08 – 15	Siku maalum za kukusanya malimbikizo ya mchango wa Tahrik Jadid na Waqfe Jadid.
		30	**Shura ya Kitaifa Dar es Salaam – mwaka 2016.**
MEI	2016	1	
		09 –16	Siku maalum za kukusanya malimbikizo ya michango. (Hasa mchango wa kawaida).
		13	Wajumbe wa Shura wayaeleze matawi yao maazimio ya Shura - 2016
		27	**Siku ya Ukhalifa.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii hii).
		27-29	**Ijtimaa ya Khuddamul Ahmadiyya Kitaifa.**
JUNI	2016	01 – 15	Siku maalum za kuhakikisha kwamba kila Mwanajumuiya amekamilisha Bajeti ya michango yake hasa wa kawaida/Wasia sawa na kiwango cha kila mwezi. Juhudi maalum zifanywe.
		3-5	**Ijtimaa na Shura ya Lajna Imaillah Kitaifa.**
		7	**Kuanza Mfungo wa saumu ya Ramadhani***

***Zingatia: Saumu ya Ramadhani, na Sikukuu zote mbili zinategemea kuandama kwa mwezi.**

Fimbo ya Mussa na Miujiza yake

Na Mwalimu Abdullah Hamisi Mbanga, Rufiji

Nabii Musa (as) anatajwa kuwa ndiye muasisi wa dhana nzima ya ukombozi katika wana wa Israeli. Musa (as) alizaliwa Misri na kukuta wana wa Israeli wakiwa katika lindi la utumwa wa kimwili na kiakili. Dhima kubwa ya ujumbe wake ilikuwa ni kuwakomboa Waisraeli kutoka katika makucha ya utawala wa Firauni uliowatweza na kuwadhalilisha kwa muda mrefu.

Akiwa mtu dhaifu aliyekosa msaada wa kibinadamu alihisi kuwa ni jukumu zito kwake kupambana na utawala wenye nguvu na dhalimu wa kimisri. Mara nyingi alimuomba sana Mola wake amtanulie kifua chake, amrahisishie jambo lake na amuondolee kifungo ulimini mwake ili watu waweze kuuelewa ujumbe wake. Si hivyo tu aliomba hata ndugu yake Haruni awe msaidizi wake katika jukumu hilo. (Kurani 20: 26 – 36).

Kutokana na jukumu hili Allah alimpa Nabii Musa (as) uwezo mkubwa wa kiroho. Alimpa uvumilivu, ujasiri na maarifa ya hali ya juu. Juu ya hayo Allah alimpa Nabii Musa (as) ishara tisa ambazo zilikuwa miujiza iliyomsaidia kuuangusha utawala wa Firauni (Kurani 7:102). Kurani Tukufu imeziainisha ishara hizo kuwa ni;

1. Fimbo yake (7:108)
2. Mkono mweupe (7:109)
3. Ukame
4. Uhaba wa matunda (7:131)
5. Tufani
6. Chawa
7. Vyura
8. ……
9. Kuvuja damu (7:134)

Kila muujiza wa Nabii una falsafa kubwa na bishara ya kimbinguni ndani yake na ndiyo maana huitwa 'AAYAAT' (Ishara). Hapa tutaangalia muujiza wake mkuu, ule wa fimbo pamoja na falsafa na bishara zilizofungamana na muujiza huo. Muujiza wa fimbo ya Nabii Musa (as) unaotajwa sehemu mbalimbali za Qurani Tukufu unasemwa kuwa ndiyo ishara kuu katika ishara zake. Qurani Tukufu inaeleza kuwa mara ya kwanza muujiza huu ulimtokea Nabii Musa (as) akiwa peke yake katika eneo la mlima wa Sinai, alipoamriwa na Allah aitupe fimbo yake ndipo ikaonekana kuwa nyoka (20:21). Muujiza huu baadaye uliwaacha vinywa wazi wachawi wa Firauni ulipofanyika mbeleyao (7:108).

Rai inayoshikwa na wengi katika muujiza huu ni kwamba fimbo iligeuka na kuwa nyoka, na kwamba alipoishika mara ya pili fimbo ilirudi katika umbo lake la kawaida. Iwapo ni kweli fimbo iligeuka kidhahiri na kuwa nyoka, jambo hili haliwezi kuwa muujiza wa kinabii, maana litakuwa limepingana na kanuni za asili za kimaumbile. Katika uumbaji wa Allah kuna kanuni zilizowekwa na kwamba kanuni hizo huwa hazivunjiki asilani na wala huwa hazina kigeugeu (35:44).



Kumbukumbu ya sanamu linaloonesha moja ya picha za Mafarao waliowahi kutawala Misri enzi za Nabii Mussa a.s.

Kwa kuwa nyoka ni kiumbe hai, Allah Anasema kuwa "Na tumefanya kutokana na maji kila kilichohai" (Kurani 21:31) ni kinyume cha kanuni za maumbile kitokane na fimbo ambayo ni kipande cha kilicho kauka ambacho yumkini hata kikipandwa hakiwezi kuota. Fimbo ile inaonekana kuwa Nabii alikuwa nayo muda mrefu kabla ya hapo aliifanyia shughuli mbalimbali (20:19).

Kama hiyo iwezekane kwamba fimbo ile ipewe uhai na kuwa "nyoka atembeaye" kama isemwavyo basi tendo la Nabii Musa (as) kuishika fimbo ile na kurudi umbile lake la awali pia linakanganya Zaidi. Maana nyoka ni miongoni mwaviumbe hai vilivyoumbwa na Allah na Kurani Tukufu inataja kuwa miongonimwa viumbe hai vitembeavyo ardhini ni wale watembeao juu ya matumbo yao (……).

Hivyo ili nyoka yule arudie tena katika umbo la fimbo isiyo na uhai, ni lazima mchakato wa kutolewa uhai ufanyike sawa na ilivyo kwa viumbe vyote vipotezavyo maisha. Kwa neno zima endapo tutachukulia muujiza huu katika maana ya kidhahiri kabisa, itakuwa sawa tu na visa vya Alifulela –u-lela ambao tunaambiwa kuna watu walikuwa wakigeuka mawe kwa kutazama tu kule walikotoka.

Ikumbukwe kwamba miujiza ya Allah haiji kama maonyesho tu ya mazingaombwe na viini macho, bali huletwa duniani kwa sababu maalum za kiroho na pia hutumika kama ishara za ukweli wa Nabii kwa vizazi vingi vijavyo, miujiza yao kubaki kuwa hai kwa karne nyingi baadaye. Kwa hivyo kama muujiza wa fimbo ya Musa ulikuwa ni kugeuka tu kwa fimbo kuwa nyoka na kuishia hapo, pasiwe hekima yoyote ndani yake, basi tendo hilo lingekuwa na tofauti gani na maonyesho ya mazingaombwe? Licha ya maelezo ya Biblia kuunga mkono dhana ya fimbo kugeuka nyoka kidhahiri. Kurani Tukufu haiungi mkono mtazamo huo. Kurani Tukufu imetumia maneno 'FALAMMAA RA-AAHAA TAHTAZZU KA-ANNAHAA JAANNU … (Na alipoiona ikitembea kana kwamba ninyoka (27:11) – hapa neno 'KA-ANNAHAA' linaashiria kuwa fimbo ilionekana kana kwamba imegeuka nyoka na haimaanishi kwamba yenyewe iligeuka nyoka kihalisia.

Bila shaka muujiza huu ulikuwa ni aina ya 'Kashf' ambayo Allah aliionyesha kwa watu wote waliokuwako kwenye tukio ambapo walijikuta wakiiona fimbo ile kuwa nyoka atambeaye. Ni kashf ambayo mara ya kwanza Musa (as) aliiona akiwa peke yake kule kwenye mlima wa Sinai (20:21) na baadaye Allah akawashirikisha Firauni na watu wake katika Kashfi hii (7:108).

Ni jambo la kawaida katika ulimwengu wa kiroho katika hali ya Kashfi mtu kuhamishwa kutoka katika maono ya kimwili na kuingia katika maono ya ulimwengu wa kiroho kwa muda. Na katika hali hiyo kila jambo analoliona huwa lina maana na taawili kubwa kuliko kama angeliona jambo hilo katika hali ya kawaida.

Hii ndiyo kusema iwapo mtu ataungua moto katika hali ya kawaida haitakuwa na maana yoyote Zaidi ya kuwa atapata tu maumivu mwilini kutokana na kidonda cha kuungua. Lakini tendo kama hilo likimtokea mtu katika hali ya Kashfi au njozi yu mkini litakuwa na maana nyingine kabisa.

Pia si jambo la ajabu kwa watu kushirikishwa katika maono mamoja kwa wakati mmoja. Hadithi zinatusimulia kwamba hata malaika Jibril ambaye alikuwa akionwa na Mtume (saw) katika Kashfi wakati fulani pia walishirikishwa masahaba wakamwona akiwa amekaa mkabala na Mtume (saw) akimuuliza baadhi ya maswali (Bukhari, kitabu Iman) hali kadhalika baadhi ya malaika walionekana hata na makafiri katika vita vya Badri (Tafsiri Ibn Jarir –J2 6, uk.47). Ni namna hii hii ya ushirikishwaji katika maono ndio uliowakuta Firauni na watu wake katika tukio la muujiza wa fimbo ya Nabii Musa (as) na si kweli kwamba kiuhalisia iligeuka kuwa nyoka.

Kwa kuwa muujiza huu ulikuwa ni maono ya Kashfi, basi kwa vyovyote utakuwa na maana kubwa na bishara ya kiungu iliyofungamana nao. Allah alipomwamuru Nabii Musa (as) atupe fimbo yake ikawa nyoka na alipoishika ikarudi kuwa fimbo inaweza kumaanisha kuwa katika lugha ya njozi na Kashfi nyoka ni adui, na fimbo huwakilisha jamii (Taatiirul Anam). Kwa hivi basi Allah alikuwa akimfahamisha Nabii Musa (as) endapo ataachana na fimbo hiyo (yaani watu wake) basi itageuka kuwa nyoka, (yaani adui), lakini kama atakuwa nao pamoja watu hao wataku wa jamii yenye nguvu na wema.

Hili pia limedhihirika katika maisha ya nabii Musa (as) pale alipoachana na watu wake kwa muda wa siku 40 alipokuwa akipewa majukumu na Allah. Watu wake waliobaki na huzuni pekee, waliunda sanamu ya ng'ombe kwa ajili ya kuiabudu (Kurani 7:149).

Aidha, Kurani Tukufu imetumia maneno matatu tofauti juu ya fimbo iliyogeuka nyoka. Maneno hayoni 'HAYYAH' (20:21), 'JAANN' (27:11) na 'THU'BAAN' (26:33). Katika hili pia kuna hekima yake. Neno'HAYYAH' - humaanisha nyoka yeyote, neno 'JAANN' – Humaanisha nyoka mdogo aghalabu anayependa kuishi katika mashimo na mapango, na neno 'THU'BAAN' humaanaisha nyoka mkubwa.

Mara nyingi muujiza huu ulipotajwa kumtokea Musa (as) akiwa peke yake neno 'JAANN' lilitumika, lakini muujiza huo ulipofanyika mbele ya Firauni na watu wake neno 'THU'BAAN' lilitumika. Hii ndiyo kusema kwamba Musa (as) endapo atashikamana na watu wake muda wote wa uhai wake basi atakapowatupa mkono (baada ya kifo chake) basi atawaacha wakiwa 'HAYYAH', neno hili pia linamaana ya kilichohai. Hivyo hii pia ilikuwa ni bishara ya kuwa taifa la Israeli litapata uhai mpya kupitia mkono wa Nabii Musa (as). Matumizi ya neno 'JAANN' muujiza huu unapomtokea Musa peke yake huashiria kuwa kuna wakati wana wa Israeli wataishi katika hali ya kujitenga na dunia huku wakipata maendeleo makubwa ya haraka, watamiliki nguvu nyingi lakini kwa kujifichaficha kwenye migongo ya mataifa au jamii nyinginezo.

Neno 'THU'BAAN' ambalo limetumika pale muujiza huo ulipodhihirika mbele ya Firauni na watu wake, linaashiria kuwa, hatimaye taifa la Israeli litajitokeza katika medani za siasa za dunia likiwa kama miongoni mwa mataifa makubwa yenye nguvu na kutishia hata usalama wa majirani zake.

Hivyo kwa muhtasari muujiza wa fimbo ya Musa ina maelezo mengi na mapana. Hii ndiyo kusema hata hali ilivyo sasa huko Mashariki ya kati kutokana na vitisho vya Israeli dhidi ya Wapalestina na mataifa jirani ni mambo yalibashiriwa zamani katika muujiza wa fimbo ya Nabii Musa (as). Zaidi ya haya kuna hekima n abishara nyingi zilizofichika katika fimbo ya Musa na miujiza yake. Allah ndiye Ajuaye Zaidi.

"Misikiti miwili na Ukombozi wa Tanzania

Na Mahmood Hamsin Mubiru, Dar es Salaam

Ni wachache sana kama wapo wanaoweza kunasibisha msikiti na ukombozi wa nchi. Kwa hakika msikiti haumkomboi mtu tu, bali unamjengea kijitambua na kufahamu sababu adhimu kwa nini ameumbwa.

Kazi hizi mbili zilifanywa kwa ufanisi na misikiti miwili iliyojengwa na Jumuiya ya Ahmadiyya nchini. Misikiti yote hii ilipata baraka ya kupewa majina na Mwana Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Bashirudin Mahmoud Ahmad r.a. Katika makala haya tutaangalia michango ya misikiti hii katika kupanda mbegu ya ukombozi.

Msikiti wa Alfazal ulifunguliwa na Sheikh Mubarak Ahmad mwaka 1944. Toka ujenzi hadi kufunguliwa yapo matukio ambayo kwa jicho makini linaweza kuona mbegu za ukombozi zikitawanywa. Msikiti huu uliyaleta makabila mengi ya Tanganyika kufanya kazi pamoja bila kujali kabila la mtu. kilichowaongoza sio kabila isipokuwa usafi wa moyo wa mtu. jambo hili haliwezi kuwa dogo ukikumbuka kuwa katika miaka ya arobaini ndipo ukoloni ulikuwa umeshika kani. Kutoka katika kila kabila hadi kwenye taifa ndio ujumbe tunaoupata katika kufanya kazi kwa pamoja na kuheshimiana. Ahmadiyya haikuwa na Waafrika peke yao, walikuwepo pia Waasia. katika siku hizi Waasia walikuwa na nafasi ya upendeleo katika jamii, wao wakahadaika na kujiona bora. Hata wakadiriki kuwabagua na kuwadharau Waafrika. Muasia asingeweza kukubali mtumie glasi moja. Ujenzi wa msikiti huo ulileta mapinduzi makubwa. Darasa la usawa lilitoka katika nadharia likajikita katika vitendo.

Waasia Waahmadiyya walishirikiana vizuri na ndugu zao wa kiroho Waafrika. Walitembeleana na Masheikh wa Kiasia walionekana kula chakula katika nyumba za Waswahili, jambo hili halikuwa dogo.

Wakati wa kusomba mawe ya msikiti huo, Waasia walikuwa bega kwa bega na Waafrika wote kwa pamoja wakibeba mawe. Kumbe hata Waasia wanaweza kubeba mawe. Si watu tofauti na sisi. Unaweza kusoma vitabu lukuki bila kuelewa dhana ya usawa na binadamu, lakini kuona ni somo kubwa.

Lakini tafrija kubwa ilikuwa kuwaona wale Waitaliano - mateka wa vita wakijenga msikiti na kulipwa. Kwa Waafrika, wazungu kazi yao ilikuwa kutawala na sio kufanya kazi hizi zilizoonekana za chini. Mshangao huu uliondoa zile fikra za kumuogopa mzungu na kumuona ni binadamu wa kawaida. Hata wale Waafrika waliopigana katika vita ya pili walirudi na fikra tofauti juu ya wazungu. Waligundua kuwa wazungu ni binadamu kama wengine. Wakifinywa wanaumia, wakichekeshwa wanacheka. Ndio maana historia ya Afrika inaonyesha mchango mkubwa wa askari waliopigana katika vita kuu ya pili.

Ufunguzi wa Al-fazal ulipambwa na nyota zinazomuelekeza binadamu katika ukombozi na usawa. Watu wa rangi zote, dini zote walikaribishwa na kukaa pamoja bila ya kutumia kigezo cha rangi, dini au kabila. Wote chini ya kivuli hicho wote

Masji Fazal Tabora - Msikiti wa kwanza wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania

waliohudhuria walikuwa sawa. Usawa unaonyeshwa na samawati inavyotanda mahali pote bila kujali hapa wanaishi matajiri na hapa wanaishi masikini. Jambo hili liliwasitua wengi. Na hakuna mfano uliokuwa umetokea wa kuwaweka Waafrika na mataifa mengine mahali pamoja katika hali ya usawa. Kumbe ni jambo linawezekana walisikika watu wakisema. Sheikh Mubarak Ahmad ameleta mambo mapya. Walizungumza mengi mara baada ya ufunguzi huo. watu walikula na kunywa pamoja. Hatua kubwa.

Siku ya ufunguzi Sheikh Mubarak Ahmad bila kuuma meno alieleza mambo ambayo kwa wakati ule ni wito wa kuibadili jamii na kuipa mwelekeo mpya. kwa sauti iliyojaa upendo aliwatangazia kuwa nyumba ile ilikuwa ni ya Allah - mmoja asiye mshirika na sote ni viumbe wake. hivyo ni lazima tutambue kwamba muumbaji wetu ni mmoja na bila shaka Allah alikuwa na shabaha ya Kutuumbia mataifa na makabila. Shabaha yenyewe ni kujuana tu, na hakuna aliye bora au mwenye heshima zaidi isipokuwa mcha Mungu. Ubora wa mtu hautokani na urefu wake au ufupi, si rangi au lugha isipokuwa mbora ni yule anayemcha Allah. Ujumbe huo uliacha wote waliohudhuria vinywa wazi. Hivyo rangi haikuwa na maana yoyote isipokuwa kwa wapaka rangi. Maneno hayo kuyatamka katika jangwa lililojaa dhuluma na uonevu ni sawasawa na kuigeuza ardhi ili iwe na rutuba na iweze kuzalisha vitu vyenye manufaa. Hotuba hiyo iliwaamsha Waafrika na hali ya kujiamini ikaanza kujengeka.

Msikiti huu ulileta mapinduzi mengine nayo ni kuipaisha lugha ya Kiswahili. misikiti mingi ilikuwa na desturi ya kutoa hotuba katika lugha ya Kiarabu na aghlabu hotuba zilizotolewa zamani zilikuwa hazina maudhui na hali halisi. Maulamaa wengi walikuwa na imani kuwa Kiswahili hakikuwa na uwezo wa kubeba fikra nzito. Wazo hilo lilifutiliwa kwa mbali na Sheikh Mubarak aliyeanza kwa hotuba ya Ijumaa kwa Kiswahili akigusia mambo ya kila siku ya mwanadamu. Hotuba hizo zikawa zinangojwa kwa hamu. Mkazo ulikuwa ni kuwajengea kujiamini waumini na kutambua matatizo yaliyokuwa yanawakabili. Ulikuwa ni uwanja wa kutoa elimu kwa jamii, kutokana na hotuba iliwezekana kuuwa ndege wawili kwa jiwe moja. Elimu na usitawishaji wa lugha ya Kiswahili hiyo ikiwa ni pamoja na tafsiri ya Quran Tukufu kwa Kiswahili, vitabu na gazeti la Mapenzi ya Mungu.

Msikiti mwingine uliofanya kazi ya ukombozi ni Masjid Salaam. Msikiti huu ulikuwa na ofisi kubwa, maktaba na ukumbi wa mkutano. Ni dhahiri ya kwamba katika miaka ya hamsini ofisi zilizokuwa na mashine ya kupiga chapa zilikuwa chache, kumbi zilikuwa chache. Kwa bahati nzuri Sheikh aliyekuwa Masjid Salaam ni yule aliyekuwa amesoma na wapigania uhuru wengi. Wapigania uhuru hao walikuwa wamepitia Tabora. Sheikh huyo alikuwa Sheikh Kaluta Amri Abedi. Mwalimu Nyerere na wanachama wengi wa TANU walifanya kazi zao masjid Salaam. Ni mahali walipopata utulivu wa kusoma vitabu na kubadilishana mawazo. Masomo pia ya Kiingereza na Kiarabu yalitolewa ambayo yaliongeza ufahamu wa wananchi. Habari walizokuwa nazo wana TANU ziliweza kutolewa katika gazeti la Mapenzi ya Mungu. Makala hizo ziliweza kutoa msisimko wa aina fulani katika mapambano dhidi ya ukoloni. Wakati wa ufunguzi mwaka 1957 walikaribishwa watu wa kila aina na falsafa ya usawa ilitolewa kwa undani. Ni katika msikiti ndipo pekee palikuwa panaheshimu mawazo ya watu wengine bila kujali itikadi yao ya dini.

Utamaduni huo wa kuheshimiana na kuvumiliana ulipewa kipaumbele na utamaduni huu ulisaidia sana katika harakati za uhuru. Mchango wa washairi hapana shaka ni mkubwa katika ukombozi wa taifa letu. Washairi wametoa mchango wao katika kuamsha jamii lakini washairi hawa walihitaji mahali pa kukutania na kubadilishana mawazo. Mahali pao palikuwa ni Masjid Salaam walipoweza kufanya mkutano wao 1959 na mkutano huo ndio uliozaa chama cha washairi. Chama kilihimiza washairi waendeleze lugha na sanaa ya ushairi. Wapenzi wa Kiswahili walikutana mara kwa mara Masjid Salaam alipokuwa anaishi Sheikh Kaluta Amri Abedi. Mikakati mingi ya kuendeleza Kiswahili ilifanyika msikitini hapa. Historia ya ukombozi wa nchi hii hauwezi kukamilika bila kutaja nafasi ya Kiswahili katika ukombozi huo. Ni dhahiri ya kwamba Kiswahili kilitoa mchango mkubwa katika ukombozi wa nchi. Hivyo yeyote aliyehusika na maendeleo ya Kiswahili alisaidia katika harakati za ukombozi wa Tanzania. Mkutano wa washairi, vitabu vingi vya Kiswahili, hivi vyote vilifanyika Masjid Salaam.

Hatimae historia ya ukombozi wa Tanzania itakapoandikwa, misikiti miwili Al-fazal Tabora na Masjid Salaam Dar es Salaam itapewa heshima maalum.

"Kiongozi wa watu ndiye Mtumishi wao"(Mtume saw)

Kutoka uk. 12

wanapopoteza maadili. Kwa kuwa kiongozi hutokana na watu, basi ni lazima watu wawe wema ili kumpata kiongozi mwema. Kurani Tukufu inaashiria hili inaposema kuwa Allah habadilishi hali za watu mpaka pale watakapobadili nafsi zao (13:12) kwa hivi basi katika uchaguzi ujao, tusitegemee kupata kiongozi mtakatifu ilhali kaumu nzima tuwahalifu.

Katika michakato ya kupata wagombea katika ngazi za vyama kulikuwa na malalamiko meng juu ya matumizi ya rushwa. Rushwa ni hara musio katika vitabu vya dini tu, bali hata katika katiba ya nchi yetu ni kosa la jinai. Lakini tumeshuhudia maafisa wa Taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa (TAKUKURU) pamoja na askari wa jeshi la polisi wakihusika kushughulikia watu kadhaa waliotuhumiwa kwa utoaji au upokeaji wa rushwa wakati wa mchakato huo.

Hapa mtu anaweza kujiuliza kwanini hivi sasa matumizi ya rushwa katika uchaguzi yamekuwa maarufu kuliko ilivyoku wazamani? Jibu lake jepesi ni hili ya kwamba jamii imemomonyoka kimaadili. Lakini kwa undani ni kwamba siasa ambayo ilianza kama kazi ya wito na ya kujitolea, sasa imekuwa ajira yenye mapato makubwa kuliko biashara nyingi nyinginezo. Ni ukweli uliowazi kwamba mshahara wa kawaida wa Mbunge ni mkubw akuliko ule wa Daktari bingwa, kama hiyo haitoshi kiinua mgongo cha Mbunge aliyetumikia kazi hiyo kwa miaka 5 pengine huwa n imara 10 zaidi ya Mwalimu, Askari au Mtumishi mwingine wa Umma aliyetumika miaka 30 kwenye ajira. Haya na mengineyo mengi yameifanya siasa kuwa siyo kazi ya uzalendo na utumishi, bali ni ajira ilipayo vizuri.

Kwa hali hii, ndiyo maana siasa imevamiwa na watu wa kila aina. Hata wasiokuwa na uwezo wa uongozi maadamu wanaweza kushawishi wapiga kura kwa vipato vyao waliacha biashara zao za kawaida na kujiunga na siasa.

Tunashuhudia Madaktari bingwa, wanasheria, Wana sayansi mahiri tena walio na ajira nzuri, wakiacha ofisi zao na kukimbilia bungeni. Hata wafanyabiashara wa kawaida nao wamejitoma katika siasa. Ingawa si wote, lakini wengi wao wamevutwa na maslahi binafsi badala ya uzalendo wa nchi. Jambo hili sasa limekuwa bayana kwa wananchi wengi na ndiyo sababu hata wapiga kura nao hudai chochote kutoka kwa wagombea, kwa kuwa wanajua kuwa kwa kumpa kura zao huwa wanampa ulaji.

Hisia hizi zinakolezwa na mabadiliko makubwa ya kiuchumi wanayoyapata wanasiasa baada ya kuingia madarakani. Ndiyo maana tumeshuhudia hamahama kubwa ya wanasiasa waliokosa uwakilishi katika vyama vyao vya zamani na kujiunga katika vyama vingine kwa lengo la kutafuta nafasi ya kugombea. Ikiwa uongozi ni utumishi, kwa nini mtu ang'ang'anie utumwa kwa gharama yoyote. Mtume Mtukufu Muhammad (saw) aliwahi kusema 'SAYYIDULQAWM HUWA KHAADIMUHUM' - yaani kiongozi wa watu ndiye mtumishi wao. Je! Hali hii ipo kwa wanasiasa wetu wa sasa? La! Hawa wa leo ni mabwana na waheshimiwa tena wenye vipato vikubwa.

Ni mpaka pale siasa itakapofanywa rasmi kuwa kazi ya kujitolea, yenye ugumu na lawama, ndipo tutakapoweza kuondokana na migogoro ya rushwa za uchaguzi. Hapo ndipo tutakapoweza kuzalisha wanasiasa waliovutwa na hamasa za kutetea wanyonge kama walivyokuwa akina Nelson Mandela, Kwame Nkurumah, Julius Kambarage Nyerere n.k hawa ni wanasiasa ambao pamoja na kushika nyadhifa kubwa kubwa katika mataifa yao walimaliza majukumu yao bila ya shutuma za kujilimbikizia mali na walikufa wakiwa watu wenye uchumi halali na wa kawaida.

Ni vyema wanasiasa wetu wakaiga mfano wa Mtume Mtukufu wa Islam (saw) ambaye pamoja na kuwa mkuu wa dola kubwa katika zama zake, alifariki akiacha nyuma yake jiwe la kusagia ngano alilokuwa akilitumia kama mto wa kulalia na matawi ya mtende aliyoyatumia kama godoro lake. Si kwamba alikuwa hana mapato la hasha! Bali alichokipata katika uongozi wake alikiingiza katika huduma za jamii kwa kuwa aliaminik wamba kiongozi ni mtumishi.

Msalieni sana Mtume s.a.w.

Kutoka uk. 12

sehemu ya juhudi hiyo atufanye kuwa miongoni mwa warithi wa baraka zilizoahidiwa kwa umma wa mtukufu Mtume s.a.w., yaani wale wenye kufanya juhudi hii.

Wakati tusomapo ***Allahumma Baarik 'alaa Muhammad,*** Tunaomba kwamba heshima ya mtukufu Mtume s.a.w. ilindwe na njama na hila za maadui zisifanikiwe. Mwenyezi Mungu ajaalie hila za maadui ziwareje wenyewe. Tunapokusanyika leo na kuomba kwa namna hii, itavutia Rehema za Mwenyezi Mungu upande wetu. Tutapata nasi baraka za kukubaliwa maombi yetu. Wakati sala zetu kwa mtukufu Mtume s.a.w. zitakapohudhurishwa mbele yake basi na maombi yetu pia yatakuwa yamekubaliwa.

Moja ya malengo makuu ya Jalsa ni kuhakikisha kwamba mapenzi ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake yanaimarika mioyoni mwetu. Lakini tutaweza tu kulifikia lengo hili iwapo tutamsalia mtukufu Mtume s.a.w. sana kutoka kwenye viini vya mioyo yetu. Na sisi wenyewe tukatenda sawa na amri za Mwenyezi Mungu na mfano ulio bora wa maisha ya mtukufu Mtume s.a.w.. Tunapomsalia mtukufu Mtume s.a.w. kwa mapenzi, jambo hilo linavutia pia mapenzi ya Mwenyezi Mungu upande wetu. Hivyo baada ya sala hii ya Ijumaa na kwa siku zingine mbili za Jalsa endeleeni kumsalia mtukufu Mtume s.a.w. kwa jazba yote ili kwamba Mwenyezi Mungu ashushe baraka juu yetu, na kwamba Mwenyezi Mungu azisukumie nyuma hila zote za maadui wetu ambazo kwa pamoja wamezikusudia juu yetu.

Katika mfano uliobarikiwa wa maisha ya mtukufu Mtume s.a.w. ulio mbele yetu tunaona jinsi alivyoweka mkazo mkubwa katika kutimiza haki za wanadamu. Basi nasi tujitahidi kuiga mfano huo. Mwenyezi Mungu Ametuagiza tuwe na huruma na tuwe wenye kuwatakia kheri wengine. Hata katika hili tunao mfano mwema wa mtukufu Mtume s.a.w. Mtukufu Mtume s.a.w. alikuwa akipata shida sana anapoona shida za waaminio. Allah ameelezea hali ya mtukufu Mtume s.a.w. ndani ya Qurani kuwa:

"Bila shaka amewafikieni Mtume kutoka miongoni mwenu; yanamhuzunisha yanayowatabisheni, anawahangaikieni (ili mpate heri), kwa waaminio ni mpole, mrehemevu." (9:128).

Basi shida za kila mmoja wetu zitufanye tusipate utulivu sawa na mfano wa mtukufu Mtume s.a.w.

Moja ya dhumuni la Jalsa ni kuongeza mafungamano yetu na hili litawezekana tu iwapo kila mmoja wetu atakuwa tayari kujitolea muhanga kwa kiwango cha hali ya juu.

Wakati Jalsa ilipoanzishwa baadhi ya watu hawakuonesha mabadiliko ya kimapinduzi kwenye tabia zao. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alihuzunishwa sana na jambo hilo na akaeleza kwamba linakatisha tamaa, na akasitisha kufanyika kwa Jalsa kwa mwaka mzima. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alitarajia udugu, mapenzi na kuhurumiana miongoni mwa wanajamaat kuongezeke kupitia mikutano ya Jalsa.

Hivi inakuwaje wale waliomwamini Masihi Aliyeahidiwa a.s. washindwe kujali juu ya shida za wengine?

Ni lazima tuzidishe mapenzi baina yetu. Ni lazima tujitahidi kupata elimu zaidi juu ya imani yetu. Marafiki wote wafike kwenye Jalsa lakini kwa lengo hili tu la kupata maendeleo zaidi ya kiimani na kiroho. Umuhimu wa Jalsa umo katika kupata maendeleo ya kiroho na kiimani. Juhudi kubwa lazima ifanyike na kila mtu ili kuhakikisha kwamba anavutia mapenzi ya Mwenyezi Mungu upande wake.

Jalsa pia inasaidia kukuza udugu na ukaribu na hilo litokeapo, faida zingine nyingi zaidi zinapatikana. Kila mmoja wetu akumbuke dhamira ya kuanzishwa kwa Jalsa na ajitahidi kukidhi vigezo na masharti ya mkutano huu. Huu si mkutano kama mikutano ya kawaida ya kidunia. Fikra zetu zote ziwe kwenye kusikiliza mazungumzo ya kidini na kiimani. Tusipoteze muda wetu kwenye mazungumzo yasiyo na maana au kuzunguka zunguka tu huku na kule kwenye mabanda ya biashara. Kuna mipango mingine pia inayoendelea nje ya ratiba kuu ya Jalsa. Badala ya kupoteza muda jaribuni kuitumia mipango hiyo ili kujiongezea elimu zaidi ya dini.

Jaribuni kuzikumbuka na kuzitafakari sana neema za Mwenyezi Mungu kwa kutimiza ahadi alizompatia Masihi Aliyeahidiwa a.s.. Jinsi gani Mwenyezi Mungu alivyofanya ili kuufikisha ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. katika kila kona ya dunia. Wakumbukeni kwenye maombi yenu mashahidi wa Jamaat hii. Na pia ombeni kwa Mwenyezi Mungu ili ailinde Jamaat dhidi ya mipango miovo ya maadui.

Pitieni machapisho ya habari za jamaat: magazeti na vitabu kwenye mabanda ya maonyesho ya vitu hivyo. Gazeti la Review of Religion limeweka banda lake maalum na pamoja na mambo mengine wanafanya maonyesho juu ya Sanda ya Yesu kwenye banda lao. Mtu anazidi kupata yakini ya ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwa kuyaona maonesho hayo. Kutaneni baina yenu. Wengi wa wanajumuiya wapya wanathibitisha kwamba kwa kadri wanavyokutana na wanajumuiya kutoka nchi mbalimbali mapenzi yao yanaongezeka zaidi.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema kwa ajili ya kukuza mapenzi yenu na ukaribu wenu, pamoja na kukua kwenu kiroho, ni lazima muzikatilie mbali kamba za vizuizi vya tofauti za tamaduni baina yenu.

Ombeaneni dua ninyi kwa ninyi ili kwamba viwango vya juu viweze kufikiwa. Mahusiano haya yawe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu. Kila mmoja wetu ajitahidi kupata faida na matunda ya kiroho yatokanayo na Jalsa. Katika siku hizi jitahidini kufikia malengo yale ya Jalsa yaliyotajwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s..

Jitahidini kuzingatia ratiba za Jalsa kwa namna ambayo itatujengea utii na utekelezaji baada ya Jalsa. Jitahidini kusikiliza hotuba kwa umakini mkubwa na katu msioneshe uvivu.
Wale ambao hawazisikilizi hotuba kwa makini hawawezi kufaidika kwazo. Kumbukeni kwamba kila kitu kinachozungumzwa ni lazima kisikilizwe kwa umakini, vinginevyo hamuwezi kupata faida yoyote. Sikilizeni kwa dhamira sio ya kujifunza tu, bali pia kutii, kukua kiimani na kujipatia faida iliyomo ndani ya yale yanayozungumzwa.

Msisikilize hotuba kwa kuvutiwa tu na mtindo wa sauti na upangaji maneno ya uzungumzaji wa mtu, bali daima zingatieni kiini cha mazungumzo ya mtoa hotuba. Wengi wa watu huvutiwa tu na mtindo wa mzungumzaji lakini hawazingatii hasa kinachozungumzwa. Masihi Aliyeahidiwa a.s. daima hakupendakabisakabisakuwa watu wavutiwe tu na mtindo wa sauti ya mzungumzaji na alikuwa akisema kuna haja gani ya kugharimika kuja kwenye Jalsa iwapo mtu hazingatii kiini cha kile kinachozungumzwa.

Mwenyezi Mungu Awajaalie washiriki wote wafaidike na Jalsa hii. Waheshimuni watoa huduma na tiini maagizo yao. Wanaohudumu wapo hapa kwa ajili ya kukusaidieni ninyi. Iwe maagizo yawe yanahusiana na jinsi ya ukaaji, au kwa ajili ya chakula, muwatii. Baadhi ya watu huhitaji huduma muda wote kutokana na sababu maalum. Basi huduma kama ya chakula iweze kupatikana muda wote. Hata hivyo kinamama waje na chakula cha watoto wao. Kila mmoja aelewe kwamba lengo la kuja hapa ni kufaidika na Jalsa.

Msongamano wa magari barabarani waweza kusababisha ucheleweshaji wa ratiba ya Jalsa, hivyo daima muwatii watu wahusikanao na usalama na muwe watulivu na wenye umakini. Maendeleo ya Jamaat pia yanavutia wivu wa maadui zetu. Hivyo tuendelee kuomba kuepushwa na shari za maadui zetu. Kwenye Jalsa kuna mipango mbalimbali iliyoelezwa kwenye ratiba basi zisomwe na zifuatwe.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. pia alisema moja ya lengo la Jalsa ni kuwakumbuka wale waliotutangulia kwenye mwaka uliopita. Hivyo leo pia nitawataja waliotutangulia hivi karibuni.

Kwanza nitaongoza sala ya Jeneza ya Mukarram Ikhramullah Sahib Shaheed kutoka Taunsa Sharif, Dera Ghazi Khan. Yeye alishambuliwa kwa risasi kwenye duka lake la madawa tarehe 19 August na kufariki hapo hapo. Wauwaji baada ya kumshambulia waliondoka kwa kasi huku wakipiga kelele za majisifu kwamba tumemuua kafiri. Alikuwa ni mtu mwema na mtawa. Alishiriki kwenye mpango wa uokoaji kwa kutoa huduma za tiba wakati wa mafuriko makubwa ya Pakistan. Alikuwa akiwasaidia dawa bure wale ambao hawakuwa na uwezo wa kununua. Alikuwa kwenye mpango wa Wasia na aliwahi kuhudumu nafasi kadhaa za kiofisi ndani ya Jamaat. Mke wake anasimulia kwamba siku kadhaa zilizopita aliwahi kupata njozi ambamo ndani yake alimuona Masihi Aliyeahidiwa a.s. akimwambia njoo haraka bila kusitasita. Mwenyezi Mungu akuze hadhi yake na aipe nguvu ya subira familia yake. Ameen.

Sala ya Jeneza ya pili ni ya Professor Muhammad Ali Sahib, aliyefariki tarehe 14 August, 2015. Alijiunga na Ahmadiyya tangu akiwa kijana. Alikuwa ni mwanajumuiya pekee kijini kwao. Alihitimu Shahada ya uzamili wa Philosofia. Aliomba kujitolea maisha yake kwa ajili ya kutumikia Jumuiya na Hadhrat Khalifatul Masih II r.a. alimkubalia maombi yake. Alikuwa akisomesha masomo mbalimbali chuoni. Alikuwa katibu muhtasi wa Khalifatul-Masih III (rh). Alikuwa pia ni Mhadhiri wa somo la Kiingereza Jamia Ahmadiyya. Ametafsiri vitabu vingi vya Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwa Kiingereza. Muhammad Ali sb. ndiye afisa wa mwanzo kuhudumu ofisi ya mpango wa Waqf-e-Nau. Kutokana na jazba yake ya kutafsiri yeye alikuwa ndie msimamizi mkuu wa Tafsiri ndani ya Jamaat (Wakil Tasneef). Aliitumikia pia seneti ya chuo Kikuu cha Punjub kwa kipindi kirefu. Alikuwa mshairi mahiri wa Kiurdu na Kipanjab na ameandika mashairi mengi. Alikuwa ni mchapa kazi sana kwani hata siku ya tarehe 13, siku moja kabla ya kufariki alikuwa ofisini akifanya kazi. Alipata tatizo la moyo kushindwa kufanya kazi na kufariki. Alikuwa na mapenzi makubwa na Ukhalifa Alikuwa akifanya kazi anazoagizwa na Khalifa kwa jazba na mapenzi ya hali ya juu na daima alikuwa akiomba Mwenyezi Mungu ampe umri ili aweze utimiza kazi anazotumwa na Khalifa.

Mwenyezi Mungu akikuze cheo chake na aijaalie Jamaat kuendelea kupata watumishi kama hao daima.

Mwisho

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Dh.Qa'da/Dh. Hj 1436 AH | Septemba 2015 | Ikha 1394 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Hakuna yeyote anisaliaye isipokuwa Mungu atanirudishia roho yangu ili nimrudishie salamu yule mwenye kunisalia (*Abu Daud*)

Khalifa Mtukufu awakumbusha Wanajumuiya:

Msalieni sana Mtume s.a.w.

Na Mwandishi Wetu

Akitoa hotuba ya Ijumaa kwenye siku ya ufunguzi wa Jalsa Salana ya Uingereza mwaka 2015, Khalifa Mtukufu alielezea juu ya haja ya kutumia nafasi ya Jalsa salana kukuza maungano zaidi na Mwenyezi Mungu kwa dhikri na kumsalia Mtume s.a.w. Katika hotuba hiyo Huzur Aqdas alisema:

Leo, Insha`Allah, baada ya Sala ya Ijumaa, Jalsa Salana ya Uingereza itafunguliwa rasmi. Sala ya Ijumaa pia inayo umuhimu wake. Ni lazima tuzingatie umuhimu huu wa sala ya Ijumaa na tuitimizie haki zake. Kwa mnasaba wa Jalsa, kutimiza haki za Ijumaa ni pamoja na kuombea baraka na mafanikio ya Jalsa.
Kuhusu umuhimu wa siku ya Ijumaa mtukufu Mtume s.a.w. alisema siku bora kabisa miongoni mwa siku zote za wiki ni Ijumaa.

...Basi nisalieni sana siku hiyo kwani sala mnazonisalia hufikishwa kwangu siku ya Ijumaa. Katika hadithi imeelezwa juu ya umuhimu wa Ijumaa kwamba kuna muda mfupi katika siku hiyo ambao dua yote iombwayo na muumini hukubaliwa, lakini muda huo ni mfupi sana.

Iwapo sisi, wakati wa hotuba, au wakati wa ibada yoyote ndani ya siku hii, tutazingatia juu ya kumsalia mtukufu Mtume s.a.w. na kusema ***Allahumma Swalii 'alaa Muhammad...,*** tufanye hivyo tukiwa na uelewa na tafakuri na kumuomba Mwenyezi Mungu kwamba aishindishe imani hii iliyoletwa na mtukufu Mtume s.a.w. duniani kote. Na pia asitawishe utukufu wake na adhama yake miongoni mwa wanadamu na kwa kuturuzuku uwezo wa kuwa

Endelea uk. 11

"Kiongozi wa watu ndiye Mtumishi wao" - Mtume s.a.w

• *Je Siasa za leo zinakidhi haja hiyo?*

Na Mwalimu Abdullah Hamisi Mbanga

Siasa ya Dunia imepita katika mawimbi mengi ya kihistoria hadi kufikia katika zama hizi tulizonazo zinazoitwa kuwa zama za demokrasia.

Historia yetu inatuonyesha kuwa kuna wakati siasa ilikuwa ni tasnia ya watu fulani maalum. Kuna nyakati koo fulani tu ndizo zilizokuwa na haki ya kufanya siasa. Penginepo baadhi ya watu kutoka familia husika na waliandaliwa tangu utotoni kwa ajili ya kuwa wanasiasa.

Ingawa huu ulikuwa ni aina ya utawala wa kifalme ambao aghalabu uliendeshwa kidikteta kwa mtazamo wa sasa wa kisiasa. Lakini kwa upande mwingine ni dola zilizodumu kwa muda mrefu na kupata mafanikio na ustawi ulioacha alama za kihistoria hadi leo.
Ni katika zama hizo ndipo walipoibuka viongozi kama Alekizanda Mkuu (Alexander the great), Kaisari, Kisra, Chengis Khan, Bukhtanassar (Nebuchadnezzer) n.k. Hawa ni miongoni mwa watu waliotawala kifalme, walikuwa wababe na wakandamizaji, lakini walifanya makubwa katika kutanua milki za utawala wao. Walijitolea kuhudumia wananchi wao, isipokuwa yule aliyejitoma kutaka kuwa Mwanasiasa bila ya ruhusa yao.

Leo hali ni tofauti, mtu yeyote anaweza kuwa Mwanasiasa, katiba za nchi zinatamka kinaga ubaga kwamba kila raia ana haki ya kuchagua au kuchaguliwa katika nafasi yoyote ya uongozi.

Vuguvugu hili lilianzia Ugiriki ambako inatajwa kuwa ndiko kwenye asili ya neno Democrasi. Wagiriki baada ya kutawaliwa kifalme kwa muda mrefu, na hatimaye wafalme kulewa madaraka na kuanza kusahau wajibu wao wa kuhudumia raia huku wakigeuka kuwa madikteta katili kwa watu wao wenyewe, Waathenia (wakazi wa kale wa Athens) kwa kutiwa hamasa na wanafalsafa wa zamani walianzisha vuguvugu la lakudai utawala unaokubalika na watu. Wakabuni usemi wao maarufu 'Vox populvox Dieco' kwamba sauti ya wengi ni sauti ya Mungu. Maana wafalme wa zamani waliwaaminisha watu kwamba wao walisimikwa na Mungu. Kuanzia wakati huo mtu aliyependekezwa na wengi wa wananchi ndiye aliyekuwa na haki ya kusimikwa kama mtawala wa nchi. Kutoka Ugiriki hamasa hiyo ilienea Ulaya na dunia nzima.

Katika nchi yetu, ambayo sasa iko katika kampeni za uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba 25 mwaka huu, Demokrasia imejikita kwa kiasi chake. Ni haki iliyo wazi kwa kila mtu kugombea nafasi yoyote ya uongozi. Ingawa bado kuna masharti kadhaa yaayovunja Demokrasia ya mtu mmoja mmoja, kama vile kutokubalika kwa wagombea binafsi.

Demokrasia ni mfumo mzuri mno katika kutoa haki kwa kila raia kuwa na kauli katika suala la utawala wa nchi yake. Raia ndiye anayeweza kuiweka au kuiondoa serikali madarakani. Huu ni utaratibu ambao mara ya kwanza kutajwa katika misahafu ilikuwa ni katika mafundisho ya Kurani Tukufu iliyotangaza kuwa 'WA UULIL AMR MINKUM' (Kurani 4:60) wenye madaraka watokane na ninyi wenyewe. Hii ilimaanisha kuwa serikali inayopaswa kutiiwa ni ile iliyotokana na wananchi wenyewe. Kwa hivi kwa mujibu wa Islam, ni halali kufanya mgomo dhidi ya udikteta na ukoloni, hata hivyo maana ya ukoloni katika Islam ni tofauti kabisa na ile inayojulikana kwa wanasiasa wa leo.
Mfumo wa kidemokrasia unalo tatizo moja kubwa ambalo hutokea pindi raia wa nchi

Endelea uk. 10